# RQF DARAJA LA 3





CCMKK302

## Mikondo yote

# Kiswahili Wastani katika Ukarimu na Utalii

**MWONGOZO WA MWANAFUNZI**

# KISWAHILI WASTANI KATIKA UKARIMU NA UTALII

2023

# AUTHOR'S NOTE PAGE (COPYRIGHT)

The competent development body of this manual is Rwanda TVET Board ©, reproduced with permission.

All rights reserved.

1. This work has been produced initially with the Rwanda TVET Board, with the support from European Union through UBUKERARUGENDO IMBERE.
2. This work is copyright, but permission is given to all the Administrative and Academic Staff of the RTB and TVET Schools to make copies by photocopying or other duplicating processes for use at their own workplaces.
3. This permission does not extend to making of copies for use outside the immediate environment for which they are made, nor making copies for hire or resale to third parties.
4. The views expressed in this version of the work does represent the views of RTB Senior Management.
5. RTB owns the copyright to the trainee and trainer's manuals. The providers of training may reproduce these guidelines in part or in full for bona fide study or in-company/workplace training purposes only. Acknowledgment of RTB copyright must be included on any reproductions. Any other use of the manuals must be referred to the RTB.

**© Rwanda TVET Board**

*Copies available from:*

- *HQs: Rwanda TVET Board-RTB*
- *Web: www.rtb.gov.rw*

**KIGALI-RWANDA**

Original published version: February 2023.

# FOREWORD

Welcome to the world of Technical and Vocational Education and Training (TVET) in the hospitality and tourism sector. In an era of constant evolution and growing demand for skilled professionals, the importance of specialized training cannot be overstated. As the global hospitality and tourism industry continues to flourish, the need for competent individuals equipped with relevant knowledge and practical skills has become crucial. This collection of TVET training manuals serves as a comprehensive resource for those seeking to embark on a fulfilling career or further their expertise within the hospitality and tourism sector. Developed with meticulous attention to detail and in collaboration with industry experts, these manuals offer a wealth of knowledge, practical insights, and hands-on training exercises. The manuals cover a wide range of topics, ranging from essential foundational concepts to specialized areas within the industry.

Whether you are interested in hotel management, culinary arts, event planning, travel and tourism, or any other facet of this vibrant sector, you will find invaluable guidance within these pages. At the heart of the TVET approach is the belief that learning should be both practical and relevant. These manuals have been carefully crafted to ensure that they reflect the real-world challenges and requirements of the hospitality and tourism industry. They are designed to empower learners with the skills, competencies, and confidence needed to excel in their chosen field.

Furthermore, the manuals adopt a learner-centered approach, encouraging active participation, critical thinking, and problem-solving. Throughout each module, learners are encouraged to engage in practical exercises, case studies, and interactive activities that simulate real-world scenarios. This hands-on approach allows learners to apply theoretical concepts and develop the necessary skills that are highly sought after in the industry.

We understand that education is a lifelong journey, and these manuals have been designed to cater to learners at various stages of their professional development. Whether you are a student taking your first steps in the industry, a working professional seeking to enhance your skills, or an instructor guiding aspiring individuals, you will find the manuals to be a valuable asset.

I would like to express my sincere appreciation to the authors, industry experts, and educators who have contributed to the creation of these TVET training manuals. Their dedication and expertise have ensured that the manuals are of the highest quality and relevance.

I encourage you to embrace the opportunities presented within these pages, to explore the dynamic world of hospitality and tourism, and to unlock your potential in this exciting industry. By investing in your education and acquiring the skills offered in these manuals, you are taking a significant step towards a rewarding and successful career.

Best wishes on your journey of discovery and growth in the hospitality and tourism sector.

**Dipl.-Ing. Paul UMUKUNZI**

**Director General/ RTB**

## SHUKRANI


Mchapishaji angependa kuwashukuru wafuatao kwa msaada wao katika utungaji wa mwongozo huu:

Bodi ya TVET ya Rwanda (RTB) inapenda kuwashukuru wahusika wote waliochangia kikamilifu katika utayarishaji wa miongozo ya mwalimu na mwanafunzi kwa mtaala huu wa Uendeshaji wa Ukarimu na Utalii wa daraja la 3 katika shule za kiufundi(TVET).

Tunapenda kutoa shukrani zetu kwa mashirika mbalimbali kama vile Umoja wa Ulaya kupitia mradi wa UBUKERARUGENDO IMBERE kwa msaada muhimu wa kifedha na kiufundi katika muda wote wa mradi. Pia tungependa kuwashukuru wataalamu wa uendeshaji wa Ukarimu na Utalii kwa mchango wao mkubwa katika mradi huu, pamoja na French Press Ltd na timu yake nzima ya uzalishaji ambayo iliendesha shughuli nzima kiufundi.

Chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya

Chini ya usimamizi na ushiriki wa UBUKERARUGENDO IMBERE

RTB | RWANDA TVET BOARD

Chini ya sera na maagizo ya Rwanda TVET Board (RTB)

# TIMU YA URATIBU

Rwamasirabo Aimable

Ntahontuye Felix

## Timu ya Uzalishaji

### Uandishi, Mapitio na Uwezeshaji

NDIKUBWAYO Faustin

MATESO Ernest

HABIYAMBERE Daniel

Faradji Gahungu

### Dhana, Urekebishaji, Uhakiki na Uhariri

Pacifique Gihozo Ngoga

Jean de Dieu Sebagabo

Samson Rukazamihigo

### Uumbizaji, Michoro na Infografiki

Albert Ngarambe

Jean Claude Asoka Niyonsaba

### Msada wa kiufundi

French Press Ltd.

# AKRONIMU

**N.K:** na kadhalika

**RTB:** Rwanda TVET Board

**TVET:** Technical and Vocational Education and Training

# YALIYOMO


Haki Miliki......................................................**Error! Bookmark not defined.**

Foreword......................................................................................... i

Shukrani ....................................................................................... iv

TIMU YA URATIBU ........................................................................... v

Akronimu....................................................................................... vi

Yaliyomo....................................................................................... vii

Utangulizi ....................................................................................... 1

**KITENGO CHA 1: KUTUMIA MSAMIATI WA KISWAHILI KATIKA MAANDISHI NA MAZUNGUMZO KIMSINGI**

Mada 1.1: Maamkizi ya aina mbalimbali na Matumizi ya herufi katika Kiswahili ..................................................................................... 10

Mada 1.2: Hesabu katika Kiswahili.............................................................. 17

Mada 1.3: Msamiati wa Mazingira tofauti .................................................... 23

**KITENGO CHA 2: KUTUMIA NA KUBAINISHA AINA ZA MANENO YA LUGHA YA KISWAHILI KIMAZUNGUMZO NA KIMAANDISHI**

Mada 2.1: Aina mbalimbali za maneno katika Kiswahili .................................. 51

Mada 2.2 Matumizi aina mbalimbali za maneno katika Kiswahili.................... 55

**KITENGO CHA 3: KUTUMIA NYAKATI ZA KISWAHILI KIMAANDISHI NA KIMAZUNGUMZO**

Mada: 3.1 Nyakati mbalimbali katika Kiswahili............................................... 76

Mada 3.2: Hali yakinishi na Hali kanushi katika Kiswahili................................ 80

Mada 3.3: Kauli za Vitenzi katika Kiswahili..................................................... 84

Marejeleo:...................................................................................... 97

# UTANGULIZI

Moduli hii inaeleza ujuzi, stadi na maadili vinavyostahiliwa ili mwanafunzi aweze kutumia Kiswahili katika ukarimu kwa kufuata stadi za lugha kama vile kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika katika shughuli za kazi.

Moduli hii inaundwa na vitengo vitatu ambavyo ni kutumia msamiati wa Kiswahili katika maandishi na mazungumzo kimsingi, kutumia na kubainisha aina za maneno ya lugha ya Kiswahili kimazungumzo na kimaandishi na kutumia nyakati za Kiswahili kimaandishi na kimazungumzo. Kila kitengo pia kinadhihirisha aina mbalimbali za tathmini na mazoezi mbalimbali yanayohamasisha mwanafunzi kuelewa umuhimu wa kutumia Kiswahili katika sekta ya Ukarimu na Utalii.

## Vitengo:

**Kitengo cha 1: Kutumia msamiati wa Kiswahili katika maandishi na mazungumzo kimsingi.**

**Kitengo cha 2 : Kutumia na kubainisha aina za maneno ya lugha ya Kiswahili kimazungumzo na kimaandishi.**

**Kitengo cha 3: Kutumia nyakati za Kiswahili kimaandishi na kimazungumzo.**

# KITENGO CHA 1: KUTUMIA MSAMIATI WA KISWAHILI KATIKA MAANDISHI NA MAZUNGUMZO KIMSINGI










## Vigezo vya Kitengo:

**1.Maamkizi, matumizi ya herufi za Kiswahili na msamiati unaofaa vinatumiwa kulingana na muktadha husika.**

**2.Hesabu za Kiswahili zinatumiwa vizuri kimazungumzo na kimaandishi kulingana na matumizi ya idadi.**

**3.Msamiati wa mazingira mbalimbali unatumiwa kwa kuzingatia muktadha husika.**

## Muhtasari wa kitengo:

Kitengo hiki kinaeleza kinagaubaga maarifa, stadi na maadili, maamkizi na matumizi ya herufi za Kiswahili kwa kuzingatia:

- ✓ Herufi za Kiswahili, irabu, konsonanti, mwambatano wa konsonanti na sauti za mkopo
- ✓ Maamkizi kulingana na wakati, rika, kuagana, kujitambulisha na maneno yanayotumiwa ya adabu na heshima
- ✓ Muda
- ✓ Hesabu za Kiswahili
- ✓ Msamiati wa mazingira tofauti ikiwemo
    - Uhusiano wa familia:
    - Sehemu za mwili
    - Majina ya wanyama
    - Aina za vyakula:
    - Mavazi
    - Usafiri

## Tathmini binafsi : kitengo cha 1

1. Tizama picha hapo juu na ujibu maswali yafuatayo:
    a) Unaona nini kwenye picha?
    b) Unafikiri nini kinatokea kwenye picha?
    c) Kielelezo kinahusiana vipi na kitengo?
    d) Je, unadhani mada gani zitajadiliwa katika kitengo hiki?

## Tathmini ya awali

1. Jaza na kamilisha jedwali la kujitathmini lililo hapa chini ili kutathmini kiwango chako cha maarifa, stadi, maadili na mitazamo chini ya kitengo hiki.
    a. Hakuna njia sahihi au zisizo sahihi za kujibu tathmini hii. Ni kwa marejeleo yako mwenyewe na kutafakari kwako mwenyewe juu ya maarifa, ujuzi na upataji wa maadili wakati wa mchakato wa kujifunza.
    b. Jifikirie : unafikiri una maarifa, stadi au maadili ya kufanya hivi ? Vipi vizuri?
    c. Soma taarifa zote hapo juu. Weka tiki kwenye safu ambayo inawakilisha vyema kiwango chako cha maarifa, stadi au maadili.
    d. Mwishoni mwa kitengo hiki, utajitathmini tena

| **Uzoefu wangu**<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi.** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi.** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili.** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kubaini aina za salamu mbalimbali zinazotumiwa katika Kiswahili kufuatana | | | | | |

| **Uzoefu wangu**<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi.** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi.** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili.** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| na nyakati mbalimbali (asubuhi, mchana, jioni). | | | | | |
| Kutaja na kurudia maneno maalumu yanayotumiwa katika kuagana | | | | | |
| Kujenga mawasiliano mema katika mazungumzo | | | | | |
| Kuonesha kwa usahihi matamshi sahihi ya sauti za Kiswahili.Kutumia vema hali kanushi na hali yakinishi | | | | | |
| Kuonyesha utamaduni wa kusalimiana, kuaga na Kuagana, na kuitikia salamu kwa usahihi. | | | | | |
| Kuhesabu vitu mbalimbali, desimali, akisami na saa | | | | | |

| **Uzoefu wangu**<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi.** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi.** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili.** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutaja aina za  majina za matunda, vyakula, mavazi na wanyama mbalimbali, aian za nafaka na usafiri | | | | | |
| Kulinganisha na kutofautisha sehemu muhimu za mwili wa mtu na kazi zake. | | | | | |

## Umahiri muhimu:

| Maarifa | Stadi | Maadili |
|---|---|---|
| 1. Kubaini aina za salamu mbalimbali zinazotumiwa katika Kiswahili kufuatana na nyakati mbalimbali (asubuhi, mchana, jioni). | **1.** Kutofautisha salamu mbalimbali kulingana na mazingira pamoja na rika na kuweza kuzitumia kwa usahihi. | **1.** Kuwa na  adabu |
| 2. Kutaja na kurudia maneno maalumu yanayotumiwa katika kuagana. | **2.** Kutumia msamiati husika kwa usahihi katika maamkizi au salamu mbalimbali, kuagana na | **2.** Kuonyesha shauku |

| Maarifa | Stadi | Maadili |
|---|---|---|
| | kuigiza katika mawasiliano | |
| 3. Kuonesha kwa usahihi matamshi sahihi ya sauti za Kiswahili. | **3.** Kugundua mabadiliko yanayojitokeza katika maneno ya salamu kama vile sijambo, hujambo, hajambo yanapokuwa katika wingi. | **3.** Kuwa msahihi |

## Kazi ya ugunduzi

**Kazi:** Mwalimu aombe wanafunzi kushuhudia michoro inayopatikana ubaoni kisha wasome mazungumzo wanayopewa

**Agaba:** Habari za asubuhi?

**Sam :** Ni nzuri, habari zako ?

**Agaba :** Nami ni nzuri

**Sam :** Vizuri. Je, unaitwa nani ?

**Agaba :** Ninaitwa Mutoni.Wewe unaitwa nani ?

**Sam:** Ninaitwa Sam, unaenda wapi?

**Agaba:** Ninaenda sokoni.

**Sam:** Kufanya nini?

**Agaba:** Ninaenda kununua matumda ya aina mbalimbali kama vile ndizi, machungwa, mapera, maparachichi, plamu, karakara pamoja na vitungu. Tena dada yangu Aganze amenituma kumununulia shati na viatu vya michezo.

**Sam:** Vizuri! Nami mama ananituma kumunulia sabuni ya kuoga. Kila sabuni inauzwa faranga mia tano za Rwanda.

**Sam:** Na mimi ni hapo, niko jirani yako. Ndipo ulipozaliwa?

**Mutoni:** Sawa tutaonana baadaye.

**Sam**: Kwa heri ya kuonana

**Mutoni:** Kwa heri

## Mada 1.1: Maamkizi ya aina mbalimbali na Matumizi ya herufi katika Kiswahili

### Kazi 1: Utatuzi wa matatizo

**Kazi**

1. Katika makundi ya wanafunzi wanne, wanafunzi wasalimiane, waagane baina yao kulingana na umri na majira ya siku.

**Mambo Muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **Maamkizi mbalimbali**
  - ✓ **Maana ya maamkizi**

Tunapozungumzia "maamkizi" huwa tunamaanisha mambo muhimu ya kuzingatia tunaposalimiana. Maamkizi ni namna ya kujuliana hali. Kwa hiyo tunapoamkiana tunapaswa kuzingatia mambo matatu yafuatayo:

- **Majira:** Nyakati za siku au wakati kitendo cha kusalimiana kinapofanywa. Yawezakuwa alfajiri, macheo, asubuhi, adhuhuri, alasiri, magharibi (machweo), jioni (usiku mchanga) au usiku wa manane.
- **Mazingira :** Ni vitu na watu vinavyomzunguka mtu mahali alipo. Yaweza kuwa ofisini, shuleni, kazini, kanisani, msikitini, darasani, shereheni, mazishini, safarini, safarini, n.k
- **Rika :** Ni kiwango cha miaka au umri wa miaka ya watu wanaoamkiana.

Iwapo watu wanaosalimiana wako katika rika moja, wanatumia maneno yanayolingana na umri wao. Lakini iwapo wanatofautiana kwa rika au umri wa miaka wanalazimika kuheshimiana kwa kutumia maneno yenyewe.

Kwa mfano : Kama mtu anayesalimia ni mdogo kuliko msalimiwa, analazimika kutumia maneno halisi ya heshima.

Kwa hiyo wanaosalimiana waweza kuwa : watoto, vijana, watu wakubwa (watu wazima), wazazi, wazee, n.k

✓ **Maamkizi ya kwaida**

- Shikamoo! Marahaba

- Nashikamoo! Kuzinawe
- Habari ya asubuhi ? Ni nzuri/salama/mbaya/njema
- Waambaje? Vema
- Hujambo? Sijambo
- Hajambo? Hajambo
- Hamjambo? Hawajambo
- Masalkheri? Aheri
- Sabalkheri? Aheri
- Cheichei! Cheichei
- Salama! Salama salimini

✓ **Namna ya kuagana**

- Kwa heri! Haya/Vizuri
- Kwa heri ya kuonana! Haya/Vizuri
- Tutaonana! Haya/Vizuri
- Tutazidi! Haya/Vizuri
- Tutaonana baadaye! Haya au Vizuri
- Alamsiki (jioni na usiku)! Bin-nuru
- Mchana mwema! Asante
- Usiku mwema! Majaliwa/Nawe pia
- Ulale salama! Asante
- Tuonane kesho! Majaliwa
- Buriani! Buriani dawa

✓ **Namna ya kumtakia mtu furaha / Faraja na Huzuni**

- **Furaha:**
    - Hongera! Nimehongera/Asante.
    - Pongezi! Asante.
- **Huzuni:**
    - Pole sana! Nishapoa
    - Poleni: Tumeshapoa
    - Makiwa! Tunayo

- **Matamshi ya herufi za Kiswahili kwa kuzingatia lafudhi**
  - ✓ **Irabu, Konsonanti na mwambatano wa konsonanti**

Lugha ya Kiswahili ina herufi za alfabeti ishirini na nne (24). Herufi hizo zinagawanyika katika makundi mawili. Kundi le kwanza ni irabu (vokali) tano (5). Kundi la pili ni konsonanti kumi na tisa (19).

Alfabeti hizo zote ni hizi zifuatazo : a,b,c,d,e,f,g,h,i,j,k,l,m,n,o,p,r,s,t,u,v,w,y,z.

Irabu au vokali

- ✓ **Irabu za Kiswahili ni tano.**

Matamshi yake ni kama yale ya lugha ya Kinyarwanda.

Mfano :

**a** : acha, angalia

**e** : endelea, embe

**i:** ingia, imba

**o**: ondoka, ondoa, ona, orodha

**u**: ukuta, ulimi, ufagio, udongo, ufa, uma, ukuta

- ✓ **Konsonanti**

Konsonanti zinazotumiwa katika lugha ya Kiswahili ni kumi na tisa.

Mifano:

b: baba, babu, bibi, bubu

c: herufi hii, haitumiwi peke yake, kila mara hufuatana na «h». hivyo hugeuka «ch».

Chuchu, chache, chotara, chura, chumba

d : dada, daftari, daktari, dari, debe

f: faida, fahali, faini, faranga, farasi, kifafa

g: goti, godoro, gorofa, gori, gazeti, gereza, goigoi

h: habari, hawara, hawala (cheki, hundi), hekima (akili, busara, ujuzi), herufi, hekalu, homa, hotuba

j: juma, joto, jina, jambazi, jana, jangwa, jela, jua

k: kaka, karamu, kalamu, kazi, katikati, karatasi, kiroboto

l: lazima, labda, lengo, leo, laini, laana, lakini, lisani, lofa, luteni, lusu (mwizi)

m: mama, mwizi, maziwa, mate, miwani, misa, moshi, moto, motokaa, mume

n: nini, nani, noma (kipingamizi), noeli, novemba, nuru

p: pua, papa, pasaka, paredi, pasi, pasipoti, papai, pole

r: ruhusa, rais, roho, rafiki, rajabu, raia, rehema, refa, riziki

s: sisi, samba, sita, sifa, sauti, sasa, soko, safari, sakafu, sufuria, sarufi, sekondari, serikali, sufuri

t: tano, tatu, timu, tembo (ndovu), tabia, takataka, tarafa, tupu, tundu

v: viti, vita, vibaya, vitamini, vokali, visu, vizuri

w: watu, waridi, wao, wakati, wapi, wewe, wilaya, wazazi, wawili, wezi, wimbo, waraka

y: yeye, Yohana, yale, yai, yaya, Yesu, yatima, Yule

z: zeze, zizi, zamani, zahanati, zaidi, ziada, zimwi, zawadi

✓ **Mwambatano wa konsonanti**

Isipokuwa irabu na konsonanti, lugha ya Kiswahili huwa na vitamkwa vinavyotokana na mfuatano au muungano wa konsonanti zaidi ya moja. Vitamkwa hivyo ni vifuatavyo:

dh, th, ch, ng', gh, ng, nn, mbw, mch, ny, sh, n.k

**Mifano:**

dh: fedha, dhambi, dhahabu, dhoruba, dharau, udhaifu, n.k

th: thelathini, themanini, thamani, themometa, theluthi, n.k

ch: chakula, mchezo, chimbuko, chotara, machozi, chura, chache, n.k

ng': kitamkwa hiki huwa na sauti ya pekee inayokaribia kufanana na jinsi tunavyotamka «nk» katika lugha ya Kinyarwanda.

ng'ombe, ng'onzi(kondoo), ng'ambo, ng'ang'ania, n.k

ng: ngozi, ngoma, ngano, nguruwe, ngamia, nguvu, n.k

gh: lugha, gharama, ghasia(fujo), ghala (stoo, bohari), ghadhabu (hasira, hamaki, ghaidhi, mafutu), ghafla, n.k

nn: nne

mbw: mbwa, mbweha(bweha)

mch: mchana, mchaguzi, mchaichai, mchakamchaka, mchoraji, mchumba, n.k

ny: nyanya, nyama, nyani, nyati(mbogo), nyumba, nyuma, nyonyo(chuchu), n.k

sh: shati, shule, shughuli, shuka, shingo, sherehe

✓ **SAA**

Saa ni kifaa cha kupimia wakati. Muda wa dakika sitini

- 9:00: saa tatu kamili

- 9:05: saa tatu na dakika tano
- 9:15: saa tatu na robo
- 9 :25 : saa tatu na dakika ishirini na tano
- 9:30: saa tatu na nusu
- 9:40: saa tatu na dakika arobaini
- 9:45: saa nne kasorobo
- 9:50: saa nne kasoro dakika kumi
- 8:00: saa mbili kamili
- 7:00: saa moja kamili
- 6:00: saakumi na mbili kamili
- 10:00: saa nne kamili
- 11:00: saa tano kamili
- 12:00: saa sita kamili
- 13:00; saa saba kamili
- 14:00: saa nane kamili
- 15:00: saa tisa kamili
- 16:00: saa kumi kamil
- 17:00: saa kumi na moja kamili
- 18:00: saa kumi na mbili kamili
- 22:15: saa nne na robo za usiku
- 23:45: saa sita kasorobo za usiku

✓ **Siku za wiki (JUMA)**

Ni siku zinazojumuisha wiki nzima

- Jumamosi
- Jumapili
- Jumatatu
- Jumanne
- Jumatano
- Alhamisi
- Ijumaa
- Jumamosi

- Jumapili

- ✓ **Miezi ya Mwaka**

Mwezi una majuma manne. Juma moja ina siku saba na mwaka una miezi kumi na miwili

Haya yafuatayo ni majina ya miezi katika Kiswahili:

- Mwezi wa kwanza = Januari
- Mwezi wa pili = Februari
- Mwezi wa tatu = Machi
- Mwezi wa nne = Aprili
- Mwezi wa tano = Mei
- Mwezi wa sita = Juni
- Mwezi wa saba = Julai
- Mwezi wa nane = Agosti
- Mwezi wa tisa = Septemba
- Mwezi wa kumi = Oktoba
- Mwezi wa kumi na moja = Novemba
- Mwezi wa kumi na mbili = Disemba

## Kazi 2: Mwongozo wa kivitendo

**Kazi: Toa majibu kwa maneno yafuatayo,**

i. Shikamoo?..........................
ii. Alamski?............................
iii. Pole!..................................
iv. Makiwa!............................
v. Hujambo?....................
vi. Sabalkheri?..................
vii. Chewa?...............................
viii. Cheichei....................
ix. Nashikamoo? ...............
x. Hamjambo?........................

Mwalimu atawasaidiya mtakapo patwahida yoyote

**Kazi 3:**

**Kazi: Utendaji Kazi katika jozi, wanafunzi wataje na wabainishe**

a) Kubainisha miezi ya mwaka

b) Kuorodhesha irabu zote za Kiswahili

c) Kuandika maneno angalau matano yanayokuwa na mwambatano wa konsonanti

d) Sasa ni saa ngapi ?

   i. 8:45:

   ii. 11:24:

e) Taja siku za Juma nzima

f) Taja mwezi unaopatikana kati ya Juni na Agosti.

## Mada 1.2: Hesabu katika Kiswahili

### Kazi 1: Utatuzi wa matatizo

**Kazi**

1. Katika makundi ya wanafunzi wanne, wanafunzi waanze kuhesabu vifaa vinavyopatikana darasani mwao.

**Mambo Muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **Hesabu katika Kiswahili**
  - ✓ **Tarakimu**

Tarakimu ni alama ya hesabu iliyoandikwa kuonyesha idadi. Kuna aina mbili za tarakimu yaani tarakimu za Kiarabu (0,1,2,3, 4,) na tarakimu za Kirumi (I, II, III,……)

- 0: Sufuri
- 1: moja
- 2: mbili
- 3: tatu
- 4: nne
- 5: tano
- 6: sita
- 7: saba
- 8: nane
- 9: tisa
- 10: kumi
- 11: kumi na moja
- 12: kumi na mbili
- 13: kumi na tatu
- 14: kumi na nne
- 15: kumi na tano
- 16: kumi na sita

- 17: kumi na saba
- 18: kumi na nane
- 19: kumi na tisa
- 20: ishirini
- 21: ishirini na moja
- 22: ishirini na mbili
- 10: kumi
- 20: ishirini
- 30: thelathini
- 40: arobaini
- 50: hamsini
- 60: sitini
- 70: sabini
- 80: themanini
- 90: tisini
- 100: mia moja
- 101: mia moja na moja
- 102: mia moja na mbili
- 200: mia mbili
- 300: mia tatu
- 400: mia nne
- 500: mia tano
- 600: mia sita
- 700: mia saba
- 800: mia nane
- 900: mia tisa
- 1000: elfu moja
- 1,001: elfu moja na moja
- 1,002: elfu moja na mbili
- 1,010: elfu moja na kumi
- 1,011: elfu moja na kumi na moja

- 1,028: elfu moja ishirini na nane
- 1,100: elfu moja na mia moja
- 1,101: elfu moja na miamoja na moja
- 1,999: elfu moja, mia tisa tisini na tisa
- 2,000: elfu mbili
- 3,000: elfu tatu
- 4,000: elfu nne
- 5,000: elfu tano
- 6,000: elfu sita
- 7,000: elfu saba
- 8,000: elfu nane
- 9,000: elfu tisa
- 10,000: elfu kumi
- 100,000: elfu mia moja au laki moja
- 200,000: elfu mia mbili au laki mbili
- 1,000,000: milioni moja
- 1,000,000,000: bilioni moja
- 1, 234, 567,890: Bilioni moja, milioni mia mbili thelathini na nne, laki tano sitini na saba, mia nane na tisini.
- 592,325: laki tano, tisini na mbili, mia tatu ishirini na tano.

✓ **DESIMALI**

- 1.1: moja nukta moja
- 1.2: moja nukta mbili
- 1.25: moja nukta mbili tano
- 5.1105: tano nukta moja moja sufuri tano
- 10.1: kumi nukta moja
- 100.15: mia moja nukta moja tano

✓ **SEHEMU (AKISAMI)**

- ½: nusu
- 1/3: theluthi moja
- 2/3: theluthi mbili

- ¼:  robo
- 1/6: sudusi
- 1/5: Humusi moja
- 1/7:  Subui moja
- 2/7: Subui mbili
- 1/10:  Ushuri moja
- 1/8: Thumuni moja
- 1/9: Tusui moja
- 2/10:  Ushuri mbili (mbili kwa kumi)
- 25/750: ishirini na tano kwa mia saba na hamsini

✓ **Asilimia**

- 20%: asilimia ishirini
- 50%: asilimia hamsini
- 25%: asilimiaishirini na tano
- 78%: asilimia sabini na nane

✓ **Alama za Hesabu**

- **+** (Alama ya kujumlisha)

✓ - (alama ya kutoa au kuondoa)

- X (alama ya kuzidisha)
- ÷ Alama ya kugawanya (kugawa)
- = Alama ya kusawazisha (alama ya sawa sawa)
- % (Alama ya asilimia)
- < (Alama ya ndogo kuliko)
    - ➢ (Alama ya kubwa kuliko)
- () (Alama ya mabano au kifungio) au mabano ya mduara
- [ ] Mabano ya mraba
- / Alama ya mkwaju

## Kazi 2: Mwongozo wa kivitendo

**Kazi: 1. Andika nambari, akisami na asilimia zifuatazo kwa maneno**

a) 6/7……………………

b) 245…………………….

c) 4/6:………………….

d) 28%..................................

e) 245.567……………………….

**2. Andika kwa nambari**

a. Sudusi nne

b. Elfu hamsini na tano

c. Humisi tatu

d. Mia mbili ishirini na tatu nukta nane saba tisa

e. Laki nne elf thelathini na nne mia tatu tisini na nne

Mwalimu atawasayidiya mkitapa shida yoyote kwa kukamkilisha kazi hiyi

### Kazi 3: Utendaji

**Kazi:Taja aina nne zinazotumiwa katika hesabu**

## Mada 1.3: Msamiati wa Mazingira tofauti

### Kazi 1: Utatuzi wa matatizo

**Kazi:**

Katika makundi, wanafunzi watoe misamiati inayohusu mazingira tofauti kama vile msamiati inayohusu uhusiano wa kifamilia, sehemu za mwili, aina za matunda, vinywaji, nafaka n.k.....

**Mambo Muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **Uhusiano wa familia**

Tunapozungumzia uhusiano wa familia kuna elementi muhimu za kufuatilia au za kuzingatia:

- Baba, Mama, wazazi, Mume, Mke.
- Mvulana (mtoto wa kiume), msichana (mtoto wa kike).
- Kaka, dada, ndugu, watoto.
- Babu, nyanya (bibi), wajukuu (mjukuu).
- Mjomba, wapwa (mpwa), shangazi.
- Baba mdogo, kaka kwa baba mdogo, dada kwa baba mdogo, baba mkwe.
- Mama mkwe, shemeji, mama mdogo.

✓ **Uhusiano wa familia unatokana na pande mbili muhimu.**

Pande hizo ni kama zifuatazo :

- Uhusano wa mume, mke, watoto na ndugu kwa upande wa mume.
- Uhusiano wa mume, mke, watoto na ndugu kwa upande wa mke.

✓ **Uhusiano:**

- Babu: Ni baba mzaa wa Baba au mama.
- Nyanya (Bibi): Ni mama mzaa wa baba au mama.
- Shangazi: Ni dada ya baba wa mtu au ndugu wa kike wa baba.
- Mjomba: Ni kaka ya mama wa mtu au ndugu wa kiume wa mama (kaka wa mama).

- Wapwa: Ni watoto wa dada ya mtu ambaye ni mwanamume.
- Ndugu: Ni watoto wanaozaliwa tumbo moja. Yaani ni ndugu kwa wazazi wote wawili.
- Wazazi: Ni baba na mama wa mtu au watu.
- Mvulana: Ni mtoto wa kiume.
- Msichana: Ni mtoto wa kike (Binti).
- Binti: Ni mtoto wa kike ambaye hajaolewa au hajafunga ndoa.
- Mwanaume: Ni mtoto wa kiume (Mvulana) amabaye ameisha funga ndoa.
- Mwanamke: Ni mtoto wa kike au msichana ambaye ameisha funga ndoa, au mtoto wa jinsia ya kike.
- Mkwe (mcheja): Mzazi wa mke au mume wa mtu.
- Baba mkwe: Ni Baba wa mke au mume wa mtu.
- Mama mkwe: Ni mama wa mke au mume wa mtu.
- Baba wa kambo: Mwanamume asiyekuwa baba yako, lakini ni mume wa mama yako au anakulea tu. Yaani hamna uhusiano wa damu.
- Mama wa kambo: Mwanamke asiyekuwa mama yako, lakini ni mke wa baba yako au anakulea tu. Yaani hamna uhusiano wa damu.
- Mtoto wa kambo : Mtoto ambaye hamna uhusiano wa damu. Yaani si mtoto kutoka tumboni mwako.
- Shemeji: Ni kaka na dada ya mke au mume wa mtu.
- Mama mdogo: Ni ndugu wa kie wa mama ya mtu.
- Mjukuu: Ni mtoto wa mtoto wa mtu.
- Kitukuu (mtukuu) : Ni mtoto wa mjukuu.
- Kilembwe: Ni mtoto wa kitukuu (mtukuu).
- Kilembwekeza (kinying'inia) : Ni mtoto aliyezaliwa na kilembwe.
- Mavyaa: Jina ambalo hutumiwa katika kuitana baina ya mke na mama wa mume wake.
- Pacha: Watoto waliozaliwa kutokana na mimba moja.

✓ **SEHEMU ZA MWILI**

Kwanza, mwili wa binadamu unagawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu hizo ni: Kichwa, Kiwiliwili na miguu.

Magofu huonyesha fuvu ambalo ndilo nyumba ya ubongo kichwani; mtulinga ambao ni mfupa uzungukao shingo kwa mbele; mbavu ambazo ndizo nyumba ya moyo na viungo vingine kifuani; uti wa mgongo ambao ndio njia ya neva(mshipa wa fahamu) na kombe la bega kwa nyuma. Kadhalika, gofu pia lina fupa la mgongo ambalo huunganisha paja na kiuno; kifandugu ambacho ndicho kifupa cha mwisho kabisa cha uti wa mgongo; pia ya goti ambayo ni kifupa mbele ya goti ambacho huchezacheza kinaposhikwa; muundi ambao ni mfupa wa mbele wa miguu; mifupa ya mikono na hata jicho la miguu ambacho ni kifupa upande huu na huu wa mguu wa chini. Ni sehemu hizi basi ambazo zikiwa na nyama huitwa mwili wa binadamu.

Mwili wa binadamu una sehemu chungu nzima. Sehemu hizo, ukianza kwa juu kichwani, ni kama vile utosi, nywele, paji, komo, kogo, ushi, ukope, mashavu, uso, pua, mdomo, mwanya, kidevu, na sikio. Kama ujuavyo, utosi ni katikati ya kichwa kwa juu. Paji ni sehemu ya juu ya uso. Lakini komo na kogo ni tofauti. Komo ni paji la uso lililotokezea, nayo kogo ni sehemu ya nyuma ya kichwa hasa iliyotokezea pia. Hata hivyo, kisogo ni sehemu ya nyuma ya kichwa.

Kuna pia mdomo, pua, sikio, mashavu, kidevu, ushi(nyusi) na ukope(kope). Nyusi ni nywele za jicho kwa juu, yaani ziko juu ya jicho kidogo. Lakini kope ni nywele ziotazo kwenye kikawa cha jicho. Pia ukope ni ngozi ifunikayo jicho. Mwanya ni nafasi iliyo katikati ya meno au uwazi uliopo baina ya meno mawili hasa ya mbele. Usoni, pana jicho. Sehemu katikati ya jicho huitwa kiini cha jicho ama mboni ya jicho.

Hali kadhalika, zipo ndevu usoni. Jina ndevu ni jina la jumla lakini mtu anaweza akanyoa na kuacha mstari wa ndevu kutoka sikio hadi hili hadi jingine. Hizi huitwa sharafa. Pengine, mtu anaweza kunyoa na kuacha ndevu chini ya mdomo wa chini. Hizi nazo huitwa kionjamchuzi au kirambamchuzi. Unaweza pia kunyoa na kuacha tu ndevu za juu ya mdomo. Hizi huitwa masharubu. Nazo ndevu ziachwazo kwenye kidevu pekee, huitwa kidevu hivyo hivyo.

Ukitoka kichwani, unapata sehemu kama vile shingo, kifua, kwapa, mikono, kiganja(viganja) au kitanga, kifundo cha mkono, kiwiko(kiungo kinachounganisha kiganja na sehemu ya juu ya mkono), kitengele(sehemu ya katikati mwa kiganja), kilimbilimbi, kucha, kisugudi(kiko), vidole, bega, matiti(chuchu), mgongo, tumbo, kitovu, kinena(kinena ni sehemu ya mwili iliyo baina ya tumbo na tupu). Sehemu hii ya kinena

ndiyo inayootea manyoya ajulikanayo kwa jina la mavuzi. Chini ya kinena kidogo kuna viungo vya kijinsia, yaani uume na uke ambavyo ni mboo na mapumbu kwa mwanamume; na kuma kwa mwanamke. Makalio (matako), kiuno, paja, goti (magoti), pia ya goti au kilegesambwa, mguu (miguu), jicho la mguu (nguyu) au kifundo cha mguu, kisigino, wayo (sehemu ya chini ya mguu inayokanyaga) na vidole vya miguu.

Kitanga cha mkono kinakuwa na vidole vitano, vile vile na mguu. Vidole hivyo ni kama vifuatavyo:

-Gumba: Kidole cha mkono au mguu kilicho kinene na kifupi kuliko vingine.

-Kidole au chanda cha shahada : Kidole kinachofuata kidole gumba.

-Kidole au chanda cha kati: Kidole kinachofuata kidole cha shahada.

-Kidole au chanda cha pete: Kidole kinachopatikana kati ya kidole cha kati na cha mwisho.

-Kidole au chanda cha mwisho: Kidole kinachofuata kidole cha pete ambacho ni kidogo kuliko vingine.

Nafasi iliyoko katikati ya vidole huitwa panda.

Unaweza vile vile kupata sehemu za ndani ya mwili. Kwa mfano, kuna kaakaa ambalo ni sehemu ya juu ya kinywa. Kuna pia ulimi ambao ni kiungo cha mwili ndani ya kinywa kinachotumika kwa kuonjea, kusemea, kurambia, n.k. Halafu tena kuna meno mbalimbali kama magego, meno ya mbwa, meno ya mbele na papachi. Meno ya mbele hutumiwa kwa kukatia chakula. pia meno ya mbele yanaweza kuwa meno ya kwanza ya mtoto mchanga ambayo hung'oka yakatoka.

Meno ya mbwa ni meno yatumiwayo kwa kutafunia chakula. Meno haya huitwa hivi kwa sababu mbwa ana meno haya pekee. Lakini magego hutumiwa kwa kusagia chakula kinacholiwa.

Pengine, ndani ya mwili, kuna moyo ambao ni injini ya mwili. Halafu kuna mapafu, ini, kongosho, tumbo, utumbo mdogo, utumbo mkubwa, wengu, kibofu na figo.

Hali kadhalika, hizi ni baadhi tu ya sehemu za mwili wa binadamu, zipo nyingine ambazo hatukuzitaja na pia kumbuka kuwa si sehemu zote za mwili zilizo na majina katika Kiswahili.

- ✓ **Wanyama wafugwao na wanyama wasiofugwa**

Kwa ujumla wanyama ni viumbe vyenye uhai, hasa hasa vyenye miguu mine, visivyokuwa watu, mimea au wadudu.

Kuna aina tofauti za wanyama, wanyama hao ni kama wanyama wafugwao, yaani wanyama wa nyumbani. Kuna pia wanyama wasiofugwa, yaani wanyama waporini.

- ✓ **Wanyama wa kufugwa (wanyama howa)**

Katika wanyama wafugwao, hebu tuangalie baadhi ya wanyama hao :

- Ng'ombe: ni mnyama wa jamii ya nyati anayefugwa na hutumiwa kupata nyama, maziwa na ngozi. Pia na kwato zake hutumiwa kutengenezea gundi.
- Mbuzi: Ni mnyama anayefanana na swala, anayefugwa kwa ajili ya kutoa nyama au maziwa.
- Mbwa: Mnyama afugwaye ambaye husaidia watu kuwinda na kulinda.
- Nguruwe: Ni mnyama afugwaye aliye mnene na mfupi, mwenye pua kubwa na ndefu, miguu mifupi, mkia mfupi na ambaye waislamu huamini kuwa ni haramu.
- Kondoo: Mnyama afugwaye mkubwa kama mbuzi mwenye manyoya marefu yatengenezwayo sufu na kutoa mavazi(nguo) ya kuvalia. Anaweza pia kuitwa Ng'onzi.
- Sungura: Mnyama mdogo mwenye masikio marefu na mkia mfupi. Yaweza pia kuitwa Kitungule.
- Paka: Ni mnyama mdogo wa jamii ya chui anayefugwa nyumbani na anayependa kula panya.
- Panya: Ni mnyama kama buku mdogo mwenye pua iliyochongoka, mkia mrefu na masharubu, paka humpenda sana kama chakula chake.
- Punda: Mnyama wa jamii ya farasi mwenye miguu mifupi na mdogo zaidi kuliko farasi na hutumiwa zaidi kwa kukokota magari au kubeba mizigo.
- Farasi: Ni mnyama wa kufugwa wa jamii ya punda lakini mkubwa zaidi kuliko punda, mwenye singa shingoni na mkiani na hutumika kubeba watu, mizigo na kuvuta gari au kwenye michezo ya kukimbia.
- Ngamia: Ni mnyama mkubwa kama Twiga mwenye nundu ambaye hutumika katika safari za jangwani.

- ✓ **Wanyama wa porini (wanyama wasiofugwa)**

Wanyama wa porini au wanyama wasiofugwa nyumbani, ni wanyama wengi sana na hatuwezi kuwazungumzia wote, bali tutapitia chache tu.

- Chui: Ni mnyama wa msituni (mwituni) wa jamii ya paka lakini mkubwa na mkali mwenye madoadoa ya njano na meusi.
- Duma: Ni mnyama mkubwa wa porini mwenye umbo kama la paka na chui.
- Simba: Ni mnyama mkubwa wa porini wa jamii ya paka mwenye manyoya ya rangi majani makavu na ambaye hula nyama.
- Nyati au mbogo: Ni mnyama wa porini mkubwa mithili ya ng'ombe mwenye pembe zilizopinda kwa mbele.
- Tembo au Ndovu: Ni mnyama mkubwa sana wa porini mwenye mkonga na pembe mbili kubwa zenye thamani kubwa sana.
- Pundamilia: Ni aina ya mnyama wa porini wa jamii ya farasi mwenye miraba mieusi na mieupe mwili mzima.
- Twiga: Ni mnyama mrefu sana wa rangi ya kahawia na mabatomabato meusi na ndefu anayepatikana katika bara la Afrika.
- Sokwe au sokwemtu (gorilla): Ni mnyama wa jamii ya nyani asiyekuwa na mkia.
- Nyani: Mnyama anayefanana na tumbiri lakini mkubwa zaidi mwenye rangi ya kaki ya kijivu na ngoko (doa) nyekundu matakoni.
- Tumbiri au tumbili: Ni mnyama mdogo wa jamii ya nyani, mwenye rangi ya kijivu na nyeupe tumboni, miguuni kifuani, mwenye mkia mrefu na uso mweusi.
- Ngedere: Ni mnyama mdogo wa jamii ya nyani na tumbiri.
- Kifaru: Ni mnyama mkubwa afananaye na kiboko na mwenye kipusa usoni.
- Buku: Ni panya mkubwa na mwenye mkia mrefu kama ndezi.
- Ndezi: Mnyama wa mwituni mwenye umbo kama la panya na mkubwa kuliko panya.
- Nungu au nungunungu: Aina ya mnyama mdogo anayefanana na nguruwe kwa sura, mwenye miba mwili mzima iliyo kama vijiti vyembamba vilivyochongoka.
- Mjusi: Ni mnyama wa jamii yenye damu baridi, mdogo kuliko kenge, huishi mashimoni au miambani. Anaweza pia kuitwa lumbwi.

- Kinyonga: Mjusi anayebadirika rangi ya mwili wake ili ifanane na rangi ya mazingira alimo.
- Kobe: Ni mnyama mwenye gamba gumu, shingo fupi na aendaye polepole.
- Mbwamwitu: Mnyama wa jamii ya mbwa aishiye porini.
- Mbweha au bweha: Ni mnyama anayefanana na mbwamwitu lakini mdogo kidogo mwenye masikio marefu yaliyosimama, mdomo mrefu mwembamba na hukamata sana kuku.
- Paa: Ni mnyama wa porini aliyefanana na mbuzi, mwembamba na mdogo, mwenye rangi ya kijivu na hudhurungi mgongoni, nyeupe tumboni, pembe ndefun na mkia wa kahawia na weupe nchani.
- Swala au swara: Ni mnyama wa jamii ya kurungu na tohe afananaye na mbuzi mkubwa.
- Fisi: Ni mnyama wa mwituni mwenye ukubwa kama wa beberu, ana rangi ya kijivu na anayeaminiwa kuwa ni mwoga na anayependa kula sana mizoga. Yaweza pia kuitwa Bakaya.
- Nyoka: Ni mnyama mrefu na mwembamba mwenye magamba na asiye na miguu, anayetambaa na kutaga mayai. Huwa na sumu, hula wadudu na vinyama vidogovidogo.
- Chatu ni nyoka mkubwa na mnene anayeua kwa kujivingirisha mwili wa windo lake.
- Swila au Fira ni nyoka mwenye mate yenye sumu na ambaye huvimbisha shingo wakati wa kurusha mate yake.
- Mamba ni nyoka mweusi au wa kijani mwenye sumu kali sana.
- Bafe au Moma ni aina ya nyoka mwenye mate yenye sumu.
- Kicheche au cheche : Ni mnyama kama paka mwitu ambaye hukamata kuku.

✓ **Wanyama wa majini**

Wanyama wa majini nao wako katika aina mbalimbali. Miongoni mwa wanyama hao tunaweza kutoa mifano k.v. samaki ambaye ni kiumbe kinachoishi ndani ya maji k.v. baharini, ziwani au mtoni, chenye mapezi na mkia ambavyo ndivyo viungo vinavyomwezesha kwenda au kupumua kwa kutumia mashavu.

Wanyama hawa nao wako katika aina nyingi sana k.v. Papa ambaye ni samaki mkubwa wa baharini asiye na mamba mwenye ngozi nene ya kijivu.

Kuna pia pomboo ambaye ni samaki mkubwa wa baharini anayefanana na papa na asiye na mamba mwenye rangi ya kijivu iliyochanganyika na hudhurungi na hudaiwa kuwa hufuata vyombo vya kusafiria.

Kuna dagaa ambao ni samaki wadogowadogo. Naye kambare ni samaki wa mtoni au ziwani mwenye masharubu.

Isipokuwa aina za samaki ambazo ni nyingi, kuna pia na wanyama wengine wanaoishi majini k.v. Chura ambaye ni mnyama mdogo mwenye ngozi laini asiye na mkia ambaye anarukaruka sana akaaye katika nchi kavu na katika maji.

Kiboko naye ni mnyama mkubwa na mnene anayeishi katika maji baridi. Mamba naye ni mnyama mkubwa mwenye magamba akaaye mtoni na ziwani.

Hakika, wanyama wanaoishi majini ni wengi chungu nzima, na huu ulikuwa mdokezo tu.

- ✓ **Ndege wa kufugwa (wa nyumbani)**
  - Kuku: Ni ndege anayefugwa na anayefanana sana na kware mkubwa mwenye kutaga mayai.
  - Jogoo: Ni kuku dume. Yaweza pia kuitwa jimbi au kikwara.
  - Njiwa: Ni ndege mkubwa kuliko tetere na mwenye raangi ya kijivu au weupe usiokoza na ambaye hula nafaka. Yaweza pia kuitwa hua au hamamu.
  - Bata: Huyu ni ndege anayeweza kufugwa au akawa wa porini, ni mkubwa kuliko kuku na hupenda kukaa majini, mwenye miguu mifupi yenye utando wa ngozi katikati ya vidole unaomwezesha kuogelea majini.
  - Batamzinga: Ni ndege mkubwa afananaye na bata mwenye manyoya ya kahawia, kichwa kisicho na manyoya, na shingo yenye ngozi ya makunyanzi isiyo na manyoya.
  - Kasuku: Ni ndege mkubwa mwenye rangi nyingi anayeweza kuiga kusema kama binadamu na mara nyingi hufugwa katika nyumba.
- ✓ **Ndege wa porini**
  - Bundi au bumu: Ni ndege mkubwa arukaye usiku tu na mwenye macho makubwa yanayomwezesha kuona gizani, hudhaniwa kuwa ni

ndege mwenye kuleta kisirani au msiba. Yaweza pia kuitwa Babewana au Babewatoto.

- Kanga: Ni ndege wa jamii ya kuku anayeishi porini, mwenye rangi ya kijivu iliyokoza na madoadoa meupe.
- Tausi: Ndege mkubwa mwenye madoa ya rangi mbalimbali, k.v. buluu na kijani, ambapo dume lina mkia mpana na mrefu ambao huuchanua na kuufunga.
- Popo: Ni mnyama mdogo kipofu mwenye mbawa anayefanana na panya, hupenda kula matunda na wadudu na kuruka usiku.
- Chiriku: Ni ndege mdogo mwenye kelele sana.
- Mbayuwayu: Ni ndege mdogo mwenye rangi nyeusi na nyeupe kooni na mgongoni karibu na mkia, ana mkia mrefu mwenye panda (mgawanyiko) na mbawa zilizokaa kama upinde arukapo na hujenga kiota cha manyoya na udongo.
- Mwewe: Ndege mkubwa anayefanana na tai ambaye hukamata vifaranga vya kuku.
- Tai: Ni ndege mkubwa mwenye kucha ndefu na kali ambaye chakula chake kikuu ni mizoga.
- Kunguru: Ndege mkubwa mweusi au mwenye baka jeupe shingoni.
- Flamingo au heroe: Ni ndege mwenye miguu mirefu nyekundu, shingo ndefu na mwili wa rangi nyeupe, hupatikana kwenye maziwa.
- Korongo: Ndege mwenye shingo ndefu na miguu mirefu, mwenye kujivuna na kujinyonga kwa uzuri wake.
- Mbuni: Ni ndege mkubwa wa mbugani asiyeweza kuruka lakini anayekwenda mbio sana kwa miguu yake.

✓ **Wadudu**

Wadudu ni viumbe vidogo vyenye mbawa nne, miguu mingi na bila ya uti wa umgongo k.v. mbu, mchwa au mende.

Wadudu wako katika aina tofauti, hebu tuangalie mifano michache.

- Mbu: Huyu ni mdudu mdogo mwembamba anayefyonza damu na huweza kuambukiza maradhi k.v. malaria, matende au homa.

- Kupe: mdudu mdogo ambaye huganda kwenye miili ya wanyama na kuwafyonza damu na huambukiza magonjwa.
- Kiroboto: Ni mdudu mdogo sana anayeuma na kufyonza damu na hupenda kukaa katika vumbi, katika manyoya ya paka au ya mbwa.
- Nzi: Ni mdudu mwenye mbawa nne na hupatikana mahali penye uchafu au kinyesi na hueneza magonjwa.
- Nzige: Mdudu aina ya panzi lakini mkubwa na anayesafiri masafa marefu kwa makundi na huharibu mimea.
- Kipepeo: Mdudu mwenye umbo jembamba na mbawa pana zenye rangi mbalimbali na hupendelea kwenye maua.
- Panzi: Ni mdudu wa jamii ya nzige, mwenye umbo refu, meno meusi mawili, mbawa nne na miguu sita ambayo miwili miongoni mwake ni mikubwa zaidi na hutumika kwa kurukia na kujihami.
- Nge (scorpion): Ni mdudu wa rangi ya kahawia au nyeusi mwenye miguu minane na mkia mrefu wenye mwiba wa sumu nchani(mwishoni).
- Chawa: Ni mdudu mdogo akaaye mwa mwanadamu, hasa katika nywele na nguo chafu na humnyonya damu.
- Mchwa: Mdudu mweupe wa jamii ya chungu anayejenga kichuguu na hula sana miti na vitu vilivyotengenezwa kwa miti.
- Nyigu: Ni mdudu wa jamii moja ya nyuki anayeuma, na mwenye kiuno chembamba. Mdudu huyu yaweza pia kuitwa dondora au mavu.
- Nyuki: Mdudu mwenye mbawa nne anayeweza kuuma, anayeishi katika kikundi kwenye mzinga na hutengeneza asali na nta.
- Kombamwiko au mende: Ni mdudu wa rangi ya kahawia mwenye mbawa nne na miguu sita, anayependa kutafuna vitu k.v. karatasi, kitambaa au nafaka na apendaye kukaa sehemu za giza.
- Jongoo: Mdudu mweusi au wa kahawia mwenye miguu mingi sana.
- Sisimizi: Mdudu mdogo wa kahawia au mweusi mwenye umbo na sura kama siafu. Yaweza pia kuitwa nyenyere au chungu.
- Siafu: Ni mdudu mdogo wa jamii ya chungu anayekwenda pamoja na kundi la wenzake, mwenye rangi ya kahawia na ambaye anauma sana.

- Kunguni: Mdudu mdogo anayefyonza damu, ambaye hukaa kwenye vitanda.
- Buibui: Ni mdudu mwenye miguu minane myembamba atandazaye utando wa kukamatia nzi na wadudu wengine.

✓ **Aina za Matunda**

Matunda ni sehemu za mimea zilizo na mbegu ndani yao.Kwa lugha ya biolojia ni ovari ya ua iliyoiva.

- chungwa / machungwa
- embe / maembe
- limao / malimao;
- limau / malimau
- nanasi / mananasi
- ndimu / ndimu
- ndizi / ndizi]
- ovakado / ovakado /
- papai / mapapai
- pera / mapera
- zabibu / mizabibu
- tofaa / matofaa /
- tufaha / matufaha
- tikiti maji / tikiti maji
- chenza / machenza
- zambarau / zambarau
- nazi / nazi
- kuyu / makuyu
- nyanya / nyanya
- peya / peya
- boga / maboga
- tende / tende
- muwa / miwa]
- fenesi / mafenesi
- matunda ya karakara

- stroberi
- tomoko / matomoko
- topetope / matopetope
- stafeli / stafeli
- balungi / mabalungi
- danzi / madanzi
- ukwaju / kwaju
- kwakwa / kwakwa
- tunguja / tunguja
- mgogwe / magogwe
- pilipili / pilipili
- tende / tende
- Parachichi /Maparachichi

✓ **Mboga**

Aina za mboga kulingana na muundo wao

Tunajua kwamba mboga nyingi zina wanga kidogo. Kawaida hazizidi kalori 30 kwa gramu 100. Hii inatufanya iwe chaguo nzuri kuanzisha katika lishe yenye kalori ndogo. Shukrani kwa ukweli kwamba wao pia wana kiwango cha juu cha nyuzi, hutoa shibe kwani idadi kubwa ya chakula inachukua nafasi kubwa ndani ya tumbo lakini haina kalori yoyote. Tutaweka orodha ndogo ya mboga za kawaida ambazo zinaweza kuletwa kwenye lishe yetu kwa sababu ya kiwango chao cha wanga na nguvu yao ya kushiba:

- Chard
- Artichokes
- Broccoli
- Asparagus
- Kabichi
- Mchicha
- Lettuce
- Purslane
- Celery

Hizi ndio mboga zinazotumiwa zaidi na ambazo zinaweza kuletwa katika lishe kwani zina wanga kidogo na nyuzi nyingi

- **Vinywaji**
  - divai ya zabibu;
  - vermouth;
  - liqueurs;
  - Martini;
  - bia;
  - ngumi;
  - Visa;
  - kimwili;
  - champagne;
  - Sake na vinywaji vingine.
- **Nafaka**

Kuna aina nyingi za nafaka, na zote zina sifa zao ingawa zinafanana kabisa. Walikuwa mimea ya kwanza kufugwa na wanadamu maelfu ya miaka iliyopita, na kwa sababu hiyo tangu wakati huo wameweza kushinda kivitendo ulimwengu wote.

Kwa hivyo, leo tunajua nafaka anuwai, kati ya hizo zifuatazo zinaonekana:

- Mchele: mimea inayoizalisha inaweza kuwa ya spishi oryza sativa, ikiwa ni mchele wa Asia, u Oryza glaberrima ikiwa ni Mwafrika. Wote hufikia urefu wa hadi sentimita 120, na huendeleza shina na majani yenye laini. Ni kiungo katika mapishi mengi, kama vile paella au mchele wa Cuba, lakini pia mara nyingi hujumuishwa katika lishe ya wanyama.
- Avena: ni mbegu ya mlolongo wa mimea ya aina hiyo: Avena ya kawaida ni Avena sativa. Inakua hadi mita moja kwa urefu. Inatumika sana kama chakula cha mifugo, lakini pia hupatikana katika biskuti zingine kwa matumizi ya binadamu.
- Shayiri : shayiri ni nyasi ya spishi hordeum vulgare. Shina zake hufikia takriban mita moja au mita moja na nusu kwa urefu. Matumizi yake inayojulikana ni kutengeneza vinywaji vyenye pombe, ingawa ni muhimu pia kwa lishe ya wanyama, haswa nguruwe.

- Chozi la Ayubu : jina la kisayansi ni Coix lacryma jobi, na ni moja ya nafaka chache ambazo hazipingi baridi. Urefu wake ni takriban mita 1, na ina lanceolate, majani ya kijani kibichi. Inatumiwa kama nafaka, isipokuwa aina ya Lacryma-Jobi ambayo ina mbegu ngumu sana na hutumiwa kutengeneza shanga.
- Mtama: ni mmea wa jenasi ya Mtama ambayo hufikia urefu wa mita 1 hadi 3 kwa urefu. Inatumika kutengeneza vinywaji vyenye pombe, na pia kutoa chakula cha wanyama.
- Ngano : Ni mimea ya jenasi Triticum inayofikia kati ya mita 1 na 3 kwa urefu. Ni moja ya kilimo zaidi katika Magharibi kwa maelfu ya miaka. Pamoja nayo, mkate, biskuti, tambi, bia huandaliwa na pia hutumiwa kama nafaka ya kiamsha kinywa.

✓ **Mavazi/ Nguo na Viatu**

Mavazi huvaliwa mwilini. Yapo mavazi ya aina nyingi.

- **Rinda** - kanzu ya kike pana iliyokatwa kiunoni.
- **Kikoi** - hufungwa kiunoni na kuteremka hadi miguuni.
- **Buibui/baibui** - vazi jeusi livaliwalo juu ya nguo nyingine.
- **Ubinda** - hupitishwa baina ya mapaja.
- **Saruni** - hufungwa kiunoni na kuteremka hadi miguuni.
- **Kibwebwe/mahazamu** -hufungwa kiunoni.
- **Masombo** -Huviringwa na kufungwa kiunoni.
- **Gagulo** - kirinda kidogo.
- **Kanchiri/sidiria** - huvaliwa kifuani.
- **Kaniki** -kanga ya kujifunga wakati wa kazi.
- **Ukaya** - kitambaa cha usoni.
- **Kizibao** -koti fupi lisilo na mikono.
- **Blauzi** - nguo ifananayo na shati.
- **Kimono** -kanzu fupi ya mtindo wa Ujapani.
- **Suti** - sketi au suruali pamoja na koti ziliozofanana kwa kitambaa na rangi.
- **Gauni** - kanzu yenye marinda.

- **Bombo** -kaptura. Suruali fupi iishiayo juu ya magoti au kwenye magoti. Pia huvaliwa na wanawake.
- **Shati** -vazi la sehemu ya juu ya mwili lililo na ukosi na mikono.
- **Sweta** -fulana nzito ya sufi. Pia huvaliwa na wanawake.
- **Kitenge** - Nguo mfano wa kanga.
- **Surupwenye/ovaroli** -vazi la juu la kuzuia mavazi mengine yasichafuke wakati wa kazi. Pia huvaliwa na wanawake (bwilasuti)
- **Suruali** -vazi la kiunoni hadi kwenye jicho la mguu lenye nafasi mbili za kupenyezea miguu. Pia huvaliwa na wanawake.
- **Joho** -koti pana na refu lililo wazi sehemu ya mbele.
- **Kilemba** -Kitambaa au nguo inayozungushwa kichwani (pia wanawake huvaa).

✓ **Mavazi ya ndani**

- Kocho (jumla)
- Sidiria – wanawake
- Shimizi/kamisi – wanawake

✓ **Kofia**

- Chepeo – kofia kubwa yenye ukingo duara uliotokeza nje ("samahani jua")
- Tarbushi/kitunga – kofia yenye shada la nyuzi ndefu.
- Kidotia – kofia ya mtoto.
- Bulibuli – kofia nyeupe iliyotiwa nakshi.
- Boshori – kofia ya mtoto.

✓ **Viatu**

- Njuti, buti
- Kubadhi
- Ndara, slipa, lapa
- Pia kuna viatu viitavyo mtarawanda

✓ **Usafiri**

Usafiri kwa kawaida ni hali ama namna ya safari za chombo cha kusafiria. Zipo namna tatu za usafiri. Msafiri anaweza kutumia usafiri wa majini, wa hewani ama wa ardhini. Baadhi ya msamiati wa namna hizi z kusafiria ni sawa hata ingawa kila sehemu ina msamiati wake

wa kipekee. Ukianza na **usafiri wa majini** unapata kuwa yapo maneno fulani fulani yanayowza kutumiwa. Kwanza kabisa, kuna meli, ngalawa, mitumbi, jahazi, mashua, mtepe na kadhalika.

Pili, **upo usafiri wa hewani**. Hewani mtu hutabiri kwa ndege ama eropleni. Nazo ni ndege ni za namna namna. Zipo za biria, kama ilivyotajwa, na zipo za mizigo. Ndege hizo lazima ziendeshwe na rubani ambaye hukaa katika dungu lameropleni. Dungu la eropleni ni sehemu anayokaa rubani na mdogo wake. Katika usafiri huu wa hewani, unapata kuwa badala ya bandari kuna kiwanja cha ndege. Kiwanjani humo ndimo mlipiwamo ushuru na forodha kwa bidhaa zinazoingia ama kutoka.

Tatu, upo **usafiri wa ardhini**. Usafiri huu nao una namna zake. Unaweza ukasafiri kwa miguu na unaweza kusafiri kwa kunyonga baiskeli. Unaweza pia kusafiri kwa motokaa na unaweza kusafiri kwa gari moshi. Vile vile, upo usafiri wa ardhini wa kutumia mahamali, magari ya ng'ombe na farasi na hata ngamia. Baadhi ya usafiri huu huweza kulipiwa nauli nao mwingine haulipiwi kutegemea anayeutumia.

## Kazi 2: Mwongozo wa kivitendo

**Kazi: Katika makundi ya wanafunzi watano**

a. Tajeni majina ya uhusiano wa familia
b. Bainisheni sehemu muhimu za mwili
c. Toeni angalau majina matano ya wanyama wafuguao na wasiofugwa
d. Taja aina tano za matunda
e. Tajeni aina tatu za usafiri

Mwalimu atakuwa nanyi kwa kutenda hiyi kazi

**Kazi 3: utendaji**

**Kazi:** Katika makundi, tungeni sentensi zenye msamiati wa mazingira tofauti.

## Tathmini Endelezi

**1. Jaza jedwali ifuatayo kwa kutumia maamkizi**

| **Maamkizi** | **Jibu** |
|---|---|
| Hujambo? | |
| | **Nimehongera** |
| Usiku mwema | |
| Alamsiki | |
| | **Marahaba** |
| Makiwa | |
| | **Kuzinawe** |
| Hawajambo? | |
| Sabalkheri | |
| | **Salimini** |

**2. Andika tarakimu hizi kwa maneno au kwa nambari**

a) 6/9

b) 245.555

c) Laki tatu elfu kumi na mbili hamsini na nne

d) 245,555

e) Asilimia arobaini na tano

f) 2.15 asubuhi

g) 4.50 asubuhi

h) 8.45 mchana

**3. Jaza nafasi tupu**

a) Mtoto wa mjukuu huitwa…….

b) Mwana wa shangazi au mjomba wako huitwa……

c) Mwana wa dada yako huitwa…………..

d) Mtoto wa kitukuu huitwa………….

e) Mzazi wa kiume wa mke wako huitwa………

4. Taja sehemu tano za mwili

5. Bainisha aina tano za matunda

6. Orodhesha aina tano za vinywaji

7. Eleza aina tatu za usafiri

## Mambo ya Kukumbuka

- ✓ Aina za maamkizi kulingana na wakati, rika na hali ya kuagana.
- ✓ Matumizi ya herufi katika Kiswahili.
- ✓ Hesabu katika Kiswahili zikiwemo desimali na akisami katika Kiswahili.
- ✓ Misamiati ya mazingira tofauti ikiwemo uhusiano wa kifamilia, matunda, wanyama, mavazi na vyakula tofauti.

## Kujitafakari

**Tathmini baada ya ujifunzaji na ufundishaji**

- Jaza tathmini ya kibinafsi hapa chini.
- Hakuna njia sahihi au zisizo sahihi za kujibu utafiti huu.
- Ni kwa matumizi yako mwenyewe wakati wa kozi hii.
- Fikiria juu yako mwenyewe : unafikiri unaweza kufanya hivi ? Vipi vizuri?
- Soma taarifa hizo hapo juu.
- Weka tiki kwenye safu inayowakilisha vyema hali yako.

| **Uzoefu wangu** <br><br> **Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi.** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kubaini aina za salamu mbalimbali zinazotumiwa katika Kiswahili kufuatana na nyakati mbalimbali (asubuhi, mchana, jioni). | | | | | |
| Kutaja na kurudia maneno maalumu yanayotumiwa katika kuagana | | | | | |
| Kujenga mawasiliano mema katika mazungumzo | | | | | |

| **Uzoefu wangu**<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi.** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuonesha kwa usahihi matamshi sahihi ya sauti za Kiswahili.Kutumia vema hali kanushi na hali yakinishi | | | | | |
| Kuonyesha utamaduni wa kusalimiana, kuaga na kuagana, na kuitikia salamu kwa usahihi. | | | | | |
| Kuhesabu vitu mbalimbali, desimali, akisami na saa | | | | | |
| Kutaja aina za majina za matunda, vyakula, mavazi na wanyama mbalimbali, aian za nafaka na usafiri | | | | | |
| Kulinganisha na kutofautisha sehemu muhimu za mwili wa mtu na kazi zake. | | | | | |

**Jaza jedwali hapa chini na ushirikishe matokeo na mwalimu kwa mwongozo zaidi.**

| Maeneo ya uimarishaji | Maeneo ya uboreshaji | Vitendo vinavyotakiwa ili kuboresha |
|---|---|---|
| 1.<br><br>2. | 1.<br><br>2. | 1.<br><br>2. |

# KITENGO CHA 2: KUTUMIA NA KUBAINISHA AINA ZA MANENO YA LUGHA YA KISWAHILI KIMAZUNGUMZO NA KIMAANDISHI.



## Vigezo vya kitengo:

1. **Mabainisho mazuri ya aina mbalimbali za maneno ya Kiswahili yanatumiwa kwa kufuata mtindo wake.**
2. **Aina mbalimbali za maneno ya Kiswahili zinatumiwa kimaandishi na kimazungumzo kulingana na mkutadha.**
3. **Sentensi sahihi za Kiswahili zinatungwa kimazungumzo na kimaandishi kulingana na upatanisho wa kisarufi.**

## Muhtasari wa kitengo:

Kitengo hiki kinaeleza kinagaubaga kinaeleza kinagaubaga matumizi ya iana za maneno ambazo ni:

- Nomino
- Vivumishi
- Vielezi
- Viwakilishi
- Viunganishi
- Vihisishi
- Vihusishi na Vitenzi

### Tathmini binafsi: kitengo cha 2

1. Tizama picha hapo juu na ujibu maswali yafuatayo:
   a. Unaona nini kwenye picha?
   b. Unafikiri nini kinatokea kwenye picha?
   c. Kielelezo kinahusiana vipi na kitengo?
   d. Je, unadhani mada gani zitajadiliwa katika mada hii?

**Tathmini ya awali**

1. Jaza na kamilisha jedwali la kujitathmini lililo hapa chini ili kutathmini kiwango chako cha maarifa, stadi, maadili na mitazamo chini ya mada hii.
   a. Hakuna njia sahihi au zisizo sahihi za kujibu tathmini hii. Ni kwa marejeleo yako mwenyewe na kutafakari kwako mwenyewe juu ya maarifa, ujuzi na upataji wa mitazamo wakati wa mchakato wa kujifunza.
   b. Jifikirie : unafikiri una maarifa, stadi au maadili ya kufanya hivi ? Vipi vizuri?
   c. Soma taarifa zote hapo juu. Weka tiki kwenye safu ambayo inawakilisha vyema kiwango chako cha maarifa, stadi au maadili.
   d. Mwishoni mwa kitengo hiki, utajitathmini tena.

| Uzoefu wangu<br><br>Maarifa, stadi na maadili | Sina uzoefu wowote wakufanya hivi | Ninajua kidogo kuhusu hili. | Nina uzoefu wa kufanya hivi. | Nina uzoefu kutosha kuhusu hili | Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi. |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutaja na kueleza aina mbalimbali za maneno kama yanavyotumika katika sentensi. | | | | | |
| Kubainisha aina za maneno zinazotumiwa katika sentensi. | | | | | |
| Kujenga mawasiliano mema katika mazungumzo | | | | | |
| Kutumia vema aina za maneno katika sentensi | | | | | |
| Kujenga uhusiano mwema katika maandishi ya nomino | | | | | |
| Kutumia kila aina ya maneno mahali panapofaa | | | | | |

## Umahiri muhimu

| Maarifa | Stadi | Maadili |
|---|---|---|
| 1. Kutaja na kueleza aina mbalimbali za maneno kama yanavyotumika katika sentensi. | 1. Kutumia vema aina za nomino katika sentensi | Kuwa mnyenyekevu |
| 2. Kubainisha aina za maneno zinazotumiwa katika sentensi. | 2. Kutumia kwa usahihi aina za vivumishi, vielezi na viwakilishi | Kutuliya |
| 3.Kufafanua aina ndogo ya kila aina ya maneno | 3. Kuunda vema sentensi zenye aina za maneno | kufatiliya mambo madogomadogo |

## Kazi ya ugunduzi

**Kazi :**

Kupitia kifungu cha habari kinachaondikwa chini, wanafunzi waulizwe kutaja mifano ya aina za maneno wanayoisoma na kuiandika ubaoni au kwenye karatasi zao.

**Kifungu: Maji**

Maji ni muhimu sana kwa maisha na viumbe vyote. Wanadamu,wanyama na mimea huhitaji maji. Kwa ukweli maji ni uhai, na uhai umo katika katika maji. Mimea huhitaji maji ili ipate kukua vizuri. Lakini kila mti huhitaji maji kwa kiwango chake maalumu. Baadhi ya miti huhitaji maji mengi. Miti mingine huhitaji kiasi na kuna miti inayohitaji maji kidogo.

Wanadamu huhitaji maji kwa shughuli mbalimbali kama vile kunywa, kuogea, kufulia na kupikia. Halikadhalika, wao huhitaji maji kuzimia moto unapotokea.

Watu hupata kutoka kwa mvua na pia kwa njia nyingine mbalimbali. Vijijini na mashambani, maji aghalabu hupatikana kutoka visimani au mitoni. Maji hutekwa yakawekwa katika chombo na kubebwa juu ya kichwa au mgongoni.

Maji majumbani huwekwa katika mtungi,debe, au pipa. Watu wengine hutumia mkokoteni aua magari kubebea maji iwapo wana madebe mengi.

Mijini, baadhi ya watu huuza maji kwa maarasi. Pamoja na hayo,majumba mengi siku hizi yana maji.

## Mada 2.1: Aina mbalimbali za maneno katika Kiswahili

### Kazi 1 : Utatuzi wa matatizo

**Kazi**

Katika makundi ya wanafunzi wanne, wanafunzi wajadili aina mbalimbali za maneno.

**Mambo muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **Aina mbalimbali za maneno katika Kiswahili**

Aina za maneno ya Kiswahili ni :

- ✓ Nomino
- ✓ Vivumishi
- ✓ Viwakilishi
- ✓ Vielezi
- ✓ Viunganishi
- ✓ Vihisishi
- ✓ Vihusishi
- ✓ Vitenzi
- ✓ NOMINO

Nomino ni maneno ambayo hutaja vitu. Kwa hiyo nomino hutaja majina ya watu, vitu, vyeo, dhana na hata tendo.

**Aina za nomino**

- Nomino za pekee
- Nomino za kawaida
- Nomino za dhahania
- Nomino za jamii
- Nomino zinazohesabika na zisizohesabika

- ✓ **VIVUMISHI**

Ni maneno ambayo hueleza jina

**Aina za vivumishi**

a. Vivumishi vya sifa

b. Vivumishi vionyeshi

c. Vivumishi viulizi

d. Vivumishi vya idadi

e. Vivumishi vimilikishi

f. Vivumishi visisitizi

- ✓ **VIWAKILISHI**

Ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino. Maneno hayo huwakilisha nomino.

**Aina za viwakilishi**

- Viwakilishi vya nafsi
- Vivumishi vya sifa na viwakilishi vya sifa
- Vivumishi vya idadi na viwakilishi vya idadi
- Vivumishi vionyeshi na viwakilishi vionyeshi
- Vivumishi viulizi na viwakilishi viulizi
- Vivumishi vimilikishi na viwakilishi vimilikishi

- ✓ **VIELEZI**

Ni maneno ambayo hueleza zaidi juu ya kitenzi, kielezi kingine au kivumishi.

**Aina za vielezi**

- Vielezi vya wakati
- Vielezi vya mahali
- Vielezi vya kiasi
- Vielezi vya namna
- Vielezi viigizi/onamatopia
- Vielezi viulizi

- ✓ **VIUNGANISHI**

Ni maneno ambayo hutumiwa kuunganisha vipashio mbalimbali katika Lugha. Lugha ya Kiswahili ina viunganishi vingi, kwa mfano: na, halafu, lakini, au, wala, ila, pia, tena, ili, kwa sababu, bila ya, isipokuwa, basi, kwa minajili, nk..

- ✓ **VIHISISHI**

Kihishi ni neno linalofahamisha jinsi mzungumzaji au mwamdishi anavyohisi au kujisikia moypni mwake. Neno hilo laweza kuwa mshituko, kiapo, kukubali, furaha, huzuni, mshangao au hisia nyingine yoyote. Kihisishi hufafanuliwa kwa matumizi ya alama hisi (!). Vihisishi, aghalabu huwa mwanzoni mwa sentensi na ni nadra kuwa mwishini ingawa hufanyika hivyo.

- Vihishi vya furaha: Ewaa! Oyee! Chabaa! Oyaa! Shabash!
- Vihishi vya huzuni : Pole ! Hamadi ! Makiwa!
- Vihisishi vya mshangao: Lahaula! Kumbe! Salale ! Ajabu ! Ati ! Eti ! Masalala ! Mama wee! Mamangu ee!
- Vihisishi vya mshituko : Afanalek ! La ! Lo ! Alaa ! Jamani ! Aisee!
- Vihisishi vya kiapo : Wallahi ! Billahi ! Haki ya Mungu!
- Vihishi vya kukubali: Naam! Haya! Ehh! Ohoo!

✓ **VIHUSISHI**

Kihusishi ni neno ambalo kwa kawaida hutumiwa na nomino au kiwakilishi na ambalo huzihusisha kisarufi nomino na viwakilishi hivyo na maneno mengine. Miongoni mwa vihusishi vinavyotumika sana katika Lugha ya Kiswahili ni kwa na na (ya kauli ya kutendwa).

## Kazi 2 : Mwongozo wa kivitendo

**Kazi:** mukiongozana na mwalimu , tajeni aina nne za:

a) Nomino

b) Vivumishi

c) Vielezi

## Kazi 3 : Utendaji

**Kazi:**

1. Katika jozi, undeni sentensi tano zinazokuwa na aina za maneno ya Kiswahili.
2. **Chagua neno linolofaa kwa kujaza pengo**
   a. Wanafunzi…………………mtihani wa taifa.( babili, wawili, viwili)
   b. ……………………….ni mji mkuu wa Rwanda( Kigali, kigari, Kigali)
   c. Kabalisa………. Kalisa wanakimbia sana( lakini, na, au, ingawa)
   d. Madereva wanaendesha magari yao………….( haraka, sana, mzuri)
   e. Muhire anaishi ………………Ngarambe(cha, kwa, vya)

**Muhtasari wa Kitengo:** Katika kitengo hiki tumebainisha aina za maneno ambazo ni:

- Nomino
- Vivumishi
- Viwakilishi
- Vielezi
- Viunganishi
- Vihisishi
- Vihusishi
- Vitenzi

## Mada 2.2 Matumizi aina mbalimbali za maneno katika Kiswahili

### Kazi 1 : Utatuzi wa matatizo

**Kazi**

Katika makundi ya wanafunzi wanne, wanafunzi wajadili namna ya kutumia aina mbalimbali za maneno.

**Mambo muhimu (yaliyomo elekezi)**

- ✓ **NOMINO**

Nomino ni maneno ambayo hutaja vitu. Kwa hiyo nomino hutaja majiana ya watu, vitu, vyeo, dhana na hata tendo.

**Aina za nomino**

- ✓ **Nomino za pekee**

Ni nomino ambazo hutaja vitu vya pekee. Kitu cha pekee ni kitu mahususi na ni cha pekee kwa sababu kipo chenyewe tu hapa duniani. Nomino za pekee hutaja majina ya:

- **Watu**: Juma, Omari, Tumaini, Kamana, Peter, n.k....
- **Miji:** Nairobi, Kigali, Dodoma, n.k.....
- **Nchi:** Rwanda, Uganda, Tanzania, n.k....
- **Mito:** Akagera, Tana, Nile, Akanyaru, n.k...
- **Milima:** Kilimanjaro, Everest, Muhabura, n.k...
- **Maziwa**: Kivu, Tanganyika, Victoria, Ruhondo, Muhazi, n.k...
- **Bahari**: Hindi, Atlantiki, n.k....
- **Miezi:** Machi, Juni, Oktoba, n.k.....
- **Siku za wiki**: Jumatatu, Ijumaa, Jumamosi, n.k....

- ✓ **Nomino za kawaida**

Ni nomino zinazotaja vitu vya kawaida ambavyo si vya pekee.Nomino hizi hutaja vitu ambavyo ni vingi hapa duniani. Nomino hizi zinaweza kuwa na umoja na wingi.

**Kwa mifano:**

- Kitabu/vitabu

- Mtu/watu
- Ukuta/kuta
- Jicho/macho
- Debe/madebe
- Kitanda /vitanda, n.k....

**a) Nomino za dhahania**

Ni nomino ambazo huwakilisha vitu ambavyo havina umbo halisi. Hizi ni nomino ambazo hatuwezi kuzihisi kwa kutumia vyungo vyetu au hata kama tungetumia darubini. Nomino hizi hazishikiki, hazionekani, hazinusiki, hazionjeki ha hazisikiki.

**Mifano:**

- Wivu
- Mawazo
- Wema
- Upendo
- Chuki
- Woga
- Uvumilivu
- Huruma
- Ushindi
- Furaha, n.k....

Haziwezi kupimwa kwa njia yoyote, lakini zinafikirika.

✓ **Nomino za jamii**

Ni nomino ambazo ndani yake kuna vitu vingi ; yaani imekusanya vitu vingi ndani yake. Mifano : kikosi, jeshi, bunge, kamati, timu, n.k....

✓ **Nomino zinazohesabika na zisizohesabika**

Nomino zinasohesabika ni zile ambazo kila mtu yeyote anaweza kuhesabu kama vile: vitanda, nyumba, magari, ndege, kalamu, karatasi, viatu, n.k.... ilhali zisizohesabika ni zile ambazo hatuwezi kuhesabu kama vile: maji, maziwa, mafuta, hewa, moshi, umeme, harufu, n.k.....

✓ **VIVUMISHI**

Kivumishi ni neno ambalo hueleza zidi juu ya nomino. Ni neno ambalo hufafanua kitu, hali, sifa au tendo linalowakilishwa na nomino.

**Mifano:**

- Mtoto mrefu
- Msichana mrembo
- Kitu kizuri
- watu watano

**Aina za vivumishi**

a. Vivumishi vya sifa
b. Vivumishi vionyeshi
c. Vivumishi viulizi
d. Vivumishi vya idadi
e. Vivumishi vimilikishi
f. Vivumishi visisitizi

**a) Vivumishi vya sifa**

Ni vivumishi ambavyo hueleza sifa fulani ya nomino inayovumishwa.

**Mifano:**

- Mti mrefu
- Chakula kitamu
- Mtoto mfupi
- Viti virefu
- Watoto wafupi, n.k....

**b) Vivumishi vionyeshi**

Ni vivumishi ambavyo hukuonyesha au kukuashiria kilipo kitu, mtu au jambo.

**Mifano:**

- Mtoto yule/watoto wale
- Mwanafunzi yule/wanafunzi wale
- Kitabu hiki/vitabu hivi
- Kalamu hii/kalamu hizi
- Mto huu/mito hii, n.k.....

**c) Vivumishi vya idadi**

Ni vivumishi ambavyo hututajia idadi ya nomino inayovumishwa.

**Mifano:**

- Watoto wawili
- Mti mmoja
- Wanafunzi wengi
- Walimu wachache
- Nahodha kumi.n.k.....

**d) Vivumishi viulizi**

Ni vivumishi ambavyo hutumiwa pamoja na na nomino ili kuuliza juu ya nomino hiyo

**Mifano:**

- Macho mangapi?
- Mikono ipi?
- Mtoto yupi?
- Watoto wangapi? n.k.....

**e) Vivumishi vimilikishi**

Ni vivumishi ambavyo hueleza jinsi nomino inavyomilikiwa.

**Mifano:**

- Mtoto wangu/watoto wetu
- Mwanafunzi wako/ wanafunzi wenu
- Kiti chake/ viti vyao

**f) Vivumishi vya kusisitiza**

Ni vivumishi ambavyo hutumiwa ili kusisitiza juu ya nomino iliyotajwa.

**Mifano**:

- Kitabu chenyewe
- Mwanafunzi mwenyewe
- Ng'ombe mwenyewe
- Kalamu yenyewe

✓ **VIWAKILISHI**

Ni maneno ambayo hutumiwa badala ya nomino. Maneno hayo huwakilisha nomino.

Aina za viwakilishi

**a) Viwakilishi vya nafsi**

Ni viwakilishi ambavyo hukaa badala ya majina ya watu.

Mifano :

**NAFSI**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Mimi | Sisi |
| Wewe | Ninyi/nyinyi |
| Yeye | wao |

**b) Vivumishi vya sifa na viwakilishi vya sifa**

**Mfano :**

- Wanafunzi hodari walifaulu lakini wavuvi walishindwa

**c) Vivumishi vya idadi na viwakilishi vya idadi**

**Mifano:**

- Watu watano walifariki na kumi wakajeruhiwa
- Wagonjwa wengi wamepona lakini wachache bado wanatibiwa

**d) Vivumishi vionyeshi na viwakilishi vionyeshi**

**Mfano :**

- Kiti hiki ni changu lakini kile pale ni chako

**e) Vivumishi visisitizi na viwakilishi visisitizi**

**Mfano :**

- Mnunuzi mwenyewe wa kitabu hajafika na chenyewe sijui kipo wapi.

**f) Vivumishi viulizi na viwakilishi viulizi**

**Mfano :**

- Watu wangapi wamepiga kura na wangapi hawajapiga ?

g) Vivumishi vimilikishi na viwakilishi vimilikishi

**Mfano :**

- Nyumba yenu ni ndogo lakini yetu ni kubwa tena inapendeza

✓ **VIELEZI**

Ni maneno ambayo hueleza zaidi juu ya kitenzi, kielezi kingine au kivumishi.

Mifano:

- Mwizi alipigwa sana.

- Amina ni mnene sana.
- Mwalimu anaongea upesi mno.

**Aina za vielezi**

**a) Vielezi vya wakati**

Ni vielezi ambavyo hueleza wakati ambapo tendo fulani lilifanyika au halikufanyika.

**Mifano:**

- Omondi atakuja kesho
- Iddi atakuja Jumatano
- Tutaondoka kesho alasiri
- Alifika jana usiku
- Ataondoka Machi
- Baba yake alifariki zamani
- Mama atatupa chakula punde

**b) Vielezi vya mahali**

Ni vielezi ambavyo hueleza mahali ambapo tendo fulani linafanyikia, lilifanyikia au litafanyikia.

**Mifano :**

- Walimu wamekwenda Nairobi
- Babake anaishi Kigali
- Muhire anaishi Burundi
- Amekwenda kaskazini

**c) Vielezi vya kiasi**

Ni vielezi ambavyo hueleza kiasi cha kutendwa kwa tendo fulani au kiasi cha uvumishi au uelezi.

Mifano :

- Mtoto ameshiba sana
- Dereva anaendesha haraka mno
- Ayubu ni mrefu kidogo

**d) Vielezi vya namna**

Ni vielezi ambavyo hueleza namna/jinsi tendo linavyotendwa

Mifano:

- Anatembea upesiupesi
- Anatembea harakaharaka
- Alikuja polepole
- Amevaa kizungu
- Anaimba vibaya/vizuri
- Alipigana kiume

**e) Vielezi viigizi/onamatopia**

Ni vielezi ambavyo huigiza milio ya matendo yanayotendwa.

**Kwa mifano :**

- Alianguka pu !
- Mtoto amelala fofofo
- Alitumbukia majini chubwi!
- Amelowa chepechepe

**f) Vielezi viulizi**

Ni vielezi ambavyo huuliza juu ya tendo.

Kwa mfano:

- Mwalimu anafundisha vipi?
- Mgonjwa amepelekwa wapi?
- Kagabo atarudi lini?
- Nani aliyemlea mgonjwa?
- Roza analeta nini?

✓ **VIUNGANISHI**

Ni maneno ambayo hutumiwa kuunganisha vipashio mbalimbali katika Lugha. Lugha ya Kiswahili ina viunganishi vingi, kwa mfano: na, halafu, lakini, au, wala, ila, pia, tena, ili, kwa sababu, bila ya, isipokuwa, basi, kwa minajili, nk..

**Mifano:**

- Mama na mtoto wanapendana.
- Chakula kinapikwa lakini bado hakijaiva.
- Mwizi hana aibu wala huruma.
- Tutoroke lakini turudi mapema.

- Usirudie kuiba pia usitudanganye tena.
- Nimekuandika barua kwa minajili ya kujua hali yako.
- Nimekuja tuongee ili nipate ukweli wa mambo.
- Amefanya alitakalo bila ya kustahi watu.
- Magonjwa yote yana dawa isipokuwa UKIMWI.
- Iwapo unaogopa kweli UKIMWI, basi jiepushe na uasherati.
- Ndugu wale wanateta pasipo na sababu yoyote.

✓ **VIHISISHI**

Kihishi ni neno linalofahamisha jinsi mzungumzaji au mwamdishi anavyohisi au kujisikia moypni mwake. Neno hilo laweza kuwa mshituko, kiapo, kukubali, furaha, huzuni, mshangao au hisia nyingine yoyote. Kihisishi hufafanuliwa kwa matumizi ya alama hisi (!). Vihisishi, aghalabu huwa mwanzoni mwa sentensi na ni nadra kuwa mwishini ingawa hufanyika hivyo.

**Mifano:**

- Vihishi vya furaha: Ewaa! Oyee! Chabaa! Oyaa! Shabash!
- Vihishi vya huzuni : Pole ! Hamadi ! Makiwa!
- Vihisishi vya mshangao: Lahaula! Kumbe! Salale ! Ajabu ! Ati ! Eti ! Masalala ! Mama wee! Mamangu ee!
- Vihisishi vya mshituko : Afanalek ! La ! Lo! Alaa! Jamani! Aisee!
- Vihisishi vya kiapo : Wallahi ! Billahi ! Haki ya Mungu!
- Vihishi vya kukubali: Naam! Haya! Ehh! Ohoo!

**Mifano katika sentensi**:

- Ewaa! Timu yetu imeibuka kuwa washindi.
- Pole! Ndiyo ulimwengu watu hupoteza wawapendao.
- Hamadi! Nataraji kikombe hakikuvunjika.
- Wallahi! Tena naapa, mimi sikushirikiana na wao ng'o
- Lahaula! Mbona siku hizi umechukua tabia isiyokuwa yako?
- Jamani! Watu wamekuwa na roho ngumu hata kuchomana moto.
- Salale! Unakula kana kwamba hujaona chakula maishani mwako.
- Kumbe! Na wewe pia umo.
- Alaa! watu wote hawapo nyumbani

- Ajabu! kwamba mpaka sasa wataalamu hawajagundua dawa ya UKIMWI

✓ **VIHUSISHI**

Kihusishi ni neno ambalo kwa kawaida hutumiwa na nomino au kiwakilishi na ambalo huzihusisha kisarufi nomino na viwakilishi hivyo na maneno mengine. Miongoni mwa vihusishi vinavyotumika sana katika Lugha ya Kiswahili ni kwa na na ( ya kauli ya kutendwa)

**Mifano :**

- Nilituma salamu kwa rafiki yangu.
- Tulikwenda kwa mganga wa kienyeji.
- Tutasafiri kwa ndege hadi London.
- Alikutwa amesimama karibu na nyumba
- Pili hulipiwa ada ya shule na shangazi yake.
- Watu wengi wameshikwa na Ukimwi.
- Nchi zote duniani zimepatwa na janga la korona.
- Tutanunua chakula kwa bei yoyote.
- Sabina aliolewa na Muhamad kwa hiari yake.
- Wachezaji wote walifuraha sana kwa ushindi walioupata

**Mifano mingine ni:**

- Tulisafiri kwa basi kutoka Nairobi hadi/mpaka Arusha
- Tumekaa siku mbili bila chakula
- Wazungu wengi maskini kama sisi
- Ndoa bila upendo haidumu
- Haishi katika nyumba yake

[2.2] ***https://www.academia.edu/34616035/Aina_za_maneno***

## Kazi 2 : Mwongozo wa kivitendo

1. **Kazi: mukiongozana na mwalimu, andikeni aina za vivumishi vinavyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:**

a) Kuna wanafunzi **wengi** kiwanjani.

b) Mwalimu **mwenyewe** anafuta ubao.

c) Mifugo **mikubwa** barani Afrika ni ng'ombe, farasi na ngamia.

d) Mkulima **mvumilivu** hufanikiwa.

e) Wazazi **wake** hupanda aina tofauti za matunda.

2. **Jaza pengo kwa kutumia kivumishi –enyewe:Fuata mfano**

a) Chungwa **lenyewe**

b) Pahali……..

c) Mti…….

d) Suruali….

e) Mnyama…..

f) Yatima…….

g) Kiwete……

h) Kipusa……

i) Chupa…..

j) Upanga….

k) Ufunguo…….

l) Bandari……

m) Mke…….

n) Kilemba……

o) Mteja…….

p) Ukuta……

q) Ngome…..

r) Hamali……

s) Kijana…….

t) Kabati……

## Kazi 3 : Utendaji

**Kazi:** Taja aina nne za maneno.

## Tathmini Endelezi

1. Eleza aina tano za maneno
2. Taja aina nne za nomino
3. **Jaza pengo kwa kutumia kivumishi –enyewe: Fuata mfano:Chungwa lenyewe**
    i. Pahali……..
    ii. Mti…….
    iii. Suruali….
    iv. Mnyama…..
    v. Yatima…….
4. **.Jaza pengo kwa kutumia kiulizi pi?**
    i. Kuimba…..kuliko kufurahisha?
    ii. Kuchora…….ambako kulikuvutia sana?
    iii. Upishi……..unataka?
    iv. Mbuzi…..watakaochinjwa siku ya sikukuu?
    v. Mkuki……ulipatikana ukitumiwa na mwindaji?
    vi. Unataka kutumia kitanda…………?
    vii. Neno…..linakushinda kulitamka?
    viii. Michezo….unapenda kuicheza?
    ix. Viongozi….wanawasaidia wananchi katika kulijenga taifa hili?
    x. Mfua chuma hutumia zana………katika kazi ya uhunzi ya kila siku.

## Mambo ya kukumbuka

**Katika kitengo hiki, tumebainisha aina za maneno zikiwemo nomino na aina zake, vivumishi, vielezi, viwakilishi, viunganishi, vihisishi, vihusishi pamoja na matumizi yake katika sentensi.**

## Kujitafakari

**Tathmini ya baada ya ujifunzaji na ufundishaji**

- Jaza tathmini ya kibinafsi hapa chini.
- Hakuna njia sahihi au zisizo sahihi za kujibu utafiti huu.
- Ni kwa matumizi yako mwenyewe wakati wa somo hili.
- Fikiria juu yako mwenyewe : unafikiri unaweza kufanya hivi ? Vipi vizuri?
- Soma taarifa hizo hapo chini.
- Weka tiki kwenye safu inayowakilisha vyema hali yako.

| **Uzoefu wangu**<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi.** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutaja na kueleza aina mbalimbali za maneno kama yanavyotumika katika sentensi. | | | | | |
| Kubainisha aina za maneno zinazotumiwa katika sentensi. | | | | | |
| Kujenga mawasiliano mema katika mazungumzo | | | | | |
| Kutumia vema aina za maneno katika sentensi | | | | | |
| Kujenga uhusiano mwema katika maandishi ya nomino | | | | | |

| Uzoefu wangu<br><br>Maarifa, stadi na maadili | Sina uzoefu wowote wakufanya hivi | Ninajua kidogo kuhusu hili. | Nina uzoefu wa kufanya hivi. | Nina uzoefu kutosha kuhusu hili | Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi. |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutumia kila aina ya maneno mahali panapofaa | | | | | |

**Jaza jedwali hapa chini na ushirikishe matokeo na mwalimu wako kwa mwongozo zaidi.**

| Maeneo ya uimarishaji | Maeneo ya uboreshaji | Vitendo vinavyotakiwa ili kuboresha |
|---|---|---|
| **1.**<br><br>**2.** | **1.**<br><br>**2.** | **1.**<br><br>**2.** |

# KITENGO CHA 3: KUTUMIA NYAKATI ZA KISWAHILI KIMAANDISHI NA KIMAZUNGUMZO



## Vigezo vya kitengo:

1. **Nyakati mbalimbali za Kiswahili zinabainishwa vema kulingana na mtindo wake.**
2. **Hali na Kauli za vitenzi katika Kiswahili zinatumiwa vizuri kimazungumzo na kimaandishi.**
3. **Kauli za vitenzi za Kiswahili zimetumiwa kwa usahihi.**

## Muhtasari wa kitengo:

Kitengo hiki kinaeleza kinagaubaga maarifa, stadi na maadili, na matumizi ya nyakati katika Kiswahili zikiwemo wakati uliopo, wakati uliotimilika, wakati ujao, wakati uliopita na wakati wa mazoea. Matumizi ya hali yakinishi na hali kanushi. Pia kuna kauli ya kutenda, kauli ya kutendeka kauli ya kutendesha, kauli ya kutendwa, kauli ya kujirudia n.k...

### Tathmini binafsi : kitengo cha 3

1. Tizama picha hapo juu na ujibu maswali yafuatayo:
    a. Unaona nini kwenye picha?
    b. Unafikiri nini kinatokea kwenye picha?
    c. Kielelezo kinahusiana vipi na kitengo?
    d. Je, unadhani mada gani zitajadiliwa katika kitengo hiki?

**Tathmini ya awali**

1. Jaza na kamilisha jedwali la kujitathmini lililo hapa chini ili kutathmini kiwango chako cha maarifa, stadi na maadili na mitazamo chini ya kitengo hiki.
    a. Hakuna njia sahihi au zisizo sahihi za kujibu tathmini hii. Ni kwa marejeleo yako mwenyewe na kutafakari kwako mwenyewe juu ya maarifa, ujuzi na upataji wa mitazamo wakati wa mchakato wa kujifunza.
    b. Jifikirie : unafikiri una maarifa, stadi au maadili ya kufanya hivi ? Vipi vizuri?
    c. Soma taarifa zote hapo juu. Weka tiki kwenye safu ambayo inawakilisha vyema kiwango chako cha maarifa, stadi au maadili.
    d. Mwishoni mwa kitengo hiki, utajitathmini tena.

| **Uzoefu wangu** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi** | **Ninajua kidogo kuhusu hili** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Maarifa, stadi na maadili** | | | | | |
| Kuainisha nyakati tofauti katika Kiswahili. | | | | | |
| Kutumia nyakati tofauti katika katika mazungumzo maandishi | | | | | |

| Uzoefu wangu<br><br>Maarifa, stadi na maadili | Sina uzoefu wowote wakufanya hivi | Ninajua kidogo kuhusu hili | Nina uzoefu wa kufanya hivi | Nina uzoefu kutosha kuhusu hili | Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga mawasiliano mema katika mazungumzo | | | | | |
| Kutofautisha matumizi ya hali yakinishi na hali kanushi katika mazungumzo na maandishi | | | | | |
| Kutumia vema hali kanushi na hali yakinishi | | | | | |
| Kutaja kauli mablimbali za vitenzi | | | | | |
| Kutumia kauli tofauti katika mazungumzo | | | | | |

## Umahiri muhimu

| Maarifa | Stadi | Maadili |
|---|---|---|
| 1. Kuainisha nyakati tofauti katika Kiswahili | 1. Kutumia nyakati tofauti katika katika mazungumzo maandishi | ▪ Kuwa na heshma |
| 2. Kueleza namna ukanushaji wa vitenzi unavyofanyika | 2. Kutofautisha matumizi ya hali yakinishi na hali kanushi katika mazungumzo na maandishi na kutumia vema hali kanushi na hali yakinishi | ▪ Kuwa na busara |
| 3. Kutaja kauli mbalimbali za vitenzi | 3. Kutumia kauli tofauti katika mazungumzo. | ▪ Kuwa mtulivu |

## Kazi ya ugunduzi

**Kazi:**

1. Kuomba wanafafunzi kujiunga katika makundi baadaye wakasoma kifungu cha habari kinachohusu matumizi ya nyakati na ukanushaji

**MIMI NA YOZEFU**

Jana, mimi na Yozefu tulikwenda sokoni. Sokoni tulinunua vitunguu, chumvi, pilipili, viazi vitamu, maharage na ndizi. Sisi hula viazi na maharage.

Leo asubuhi tumekwenda sokoni tena. Lakini hatukununua vitu vingi. Leo tumenunua sabuni ya kufulia na sabuni ya kuogea. Sasa mimi ninakwenda dukani kununua sigara na kiberiti. Baba huvuta sigara lakini Mama havuti. Baba hunituma dukani kila siku. Juzi alinituma kununua wembe lakini jana hakunituma wembe. Jana mama alinituma mimi na Yozefu kwenda sokoni.

Kesho mimi na dada tutakwenda shuleni. Hatutakwenda sokoni wala dukani. Tutakwenda shuleni kusoma. Tukitoka shuleni tutarudi upesi nyumbani. Baba yangu ni seremala, na mama hufanya kazi ya nyumbani. Hivi nitamsaidia mama kazi za jikoni. Dada hatamsaidia Baba.

## Mada: 3.1 Nyakati mbalimbali katika Kiswahili

### Kazi 1 : Utatuzi wa matatizo

### Kazi

1. Katika makundi ya wanafunzi wanne, wanafunzi waweke vitenzi mbalimbali katika nyakati tofauti na zitumiwe katika sentensi.

**Mambo muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **Nyakati katika Kiswahili**

Wakati, katika Kiswahili huonekana katika vitenzi. Huonyeshwa na viambishi au viwakilishi wakati ndani ya kitenzi. Katika Kiswahili kuna nyakati tano:

i. Wakati uliopo -**na**-

ii. Wakati ujao -**ta**-

iii. Wakati uliopita-**li-**

iv. Wakati wa mazoea-**hu**-

v. Wakati uliotimilika -**me**-

**Mfano: Kitenzi kupika**

**WAKATI ULIOPO (-na-)**

Wakati uliopo unatumika kwa kueleza tendo linalotendeka sasa hivi, saa hizi, muda huu. Ni wakati wa sasa. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ na+ kitenzi kilichopoteza (ku).

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mimi ninapika chakula | Sisi tunapika vyakula |
| Wewe unapika chakula | Ninyi mnapika vyakula |
| yeye anapika chakula | Wao wanapika vyakula |

- **WAKATI UJAO (-TA-)**

Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vitakavyofanyika wakati utakaokuja baadaye (future tense). Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ ta+ kitenzi kilichopoteza (ku). Maneno yanayoonyesha wakati ujao ni: kesho, keshokutwa, mtondo, mtondogoo, n.k

| **Umoja** | **WINGI** |
|---|---|
| Mimi ni**ta**pika chakula | Sisi tutapika vyakula |
| Wewe u**ta**pika chakula | Ninyi mtapika vyakula |
| Yeye a**ta**pika chakula | Wao watapika vyakula |

- **WAKATI ULIOPITA (-LI-)**

Viambishi wakati katika wakati uliopita ni –**li**- katika hali yakinishi na -**ku**- katika hali ya kukanusha. Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vilivyofanyika zamani (past tense). Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ li+ kitenzi kilichopoteza (ku). Maneno yanayoonyesha wakati uliyopita ni: Jana, juzi, juzijuzi, majuzi yale.

Mfano:

Kitenzi: kupika

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mimi nilipika chakula | Sisi tulipika vyakula |
| Wewe ulipika chakula | Ninyi mlipika vyakula |
| Yeye alipika chakula | Wao walipika vyakula |

- **WAKATI ULIOTIMILIKA (-ME-)**

Katika wakati uliotimilika tungo yakinishi, kiambishi wakati ni **-me-.** Katika wakati uliotimilika, tungo kanushi, kiambishi wakati ni **-ja**-. Maneno yanayoonyesha wakati timilifu ni **leo** na **hivi punde**

**Mfano:** Kitenzi: kufungua

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Mimi ni**me**fungua chupa | Sisi tumefungua chupa |
| Wewe u**me**fungua chupa | Ninyi mmefungua chupa |
| Yeye a**me**fungua chupa | Wao wamefungua chupa |

**TANBIHI**:

**1**. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ **me**+ kitenzi kilichopoteza (ku).

- **WAKATI WA MAZOEA (HU-)**

Katika wakati wa mazoea, kiambishi **-hu-** huchukua nafasi ya kiambishi nafsi na kiambishi wakati. Wakati wa mazoea humaanisha kutendeka kwa tendo kila siku au kila wakati. Katika kukanusha ni kama vile katika wakati uliopo.

**Mfano:** Kitenzi kutandika

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kila siku mimi hutandika kitanda | Kila siku sisi hutandika vitanda |
| Kila siku wewe hutandika kitanda | Kila siku ninyi hutandika vitanda |
| Kila siku yeye hutandika kitanda | Kila siku wao hutandika vitanda |

## Kazi 2 : Mwongozo wa Utendaji

**Kazi: 1. Weka vitenzi vilivyo mabanoni katika wakati unaofaa**

a. Leo, sisi ………………. (faulu) tathmini ya Kiswahili.
b. Wakristo ……………………(Sali) kila Jumapili
c. Mimi ………………. (lima) shamba kesho.
d. Ninyi ……………. (fanya) jaribio la Kemia sasa hivi.
e. Mwalimu wetu……………. (tutembelea) juzi.

## Kazi 3 : Utendaji

**Kazi 3.**

1. **Andika sentensi zifuatazo katika wakati unaopewa katika mabano:**
    a. Ulifanya nini kesho? (Ujao)
    b. Sikuelewa kazi waliyofanya. (uliopo)
    c. Baba hakupanda aina nyingi za matunda. (uliotimilika)
    d. Ulikuwa wapi jana? (ujao)
    e. Wazazi wa yule kijana watafika kesho. (uliopita)
2. Kuomba wanafunzi kutumia nyakati walizojifunza katika sentensi.

## Mada 3.2: Hali yakinishi na Hali kanushi katika Kiswahili

### Kazi 1 : Utatuzi wa matatizo

**Kazi**

1. Katika jozi, wanafunzi washirikiane na kujadili namna ukanushaji unavyofanyika katika Kiswahili.

**Mambo Muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **WAKATI ULIOPO (-na-)**

**Mfano:** Kitenzi kupika

| **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| Mimi ninapika chakula | Mimi sipiki chakula |
| Wewe unapika chakula | Wewe hupiki chakula |
| Yeye anapika chakula | Yeye hapiki chakula |
| Sisi tunapika chakula | Sisi hatupiki vyakula |
| Nyinyi mnapika chakula | Nyinyi hampiki vyakula |
| Wao wanapika chakula | Wao hawapiki vyakula |

**TANBIHI:**

1. Wakati uliopo unatumika kwa kueleza tendo linalotendeka sasa hivi, saa hizi, muda huu. Ni wakati wa sasa.
2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ na+ kitenzi kilichopoteza (ku).

- **WAKATI UJAO (-TA-)**

**Mfano:** Kitenzi kupika

| **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| Mimi ni**ta**pika chakula | Mimi sitapika chakula |
| Wewe u**ta**pika chakula | Wewe hutapika chakula |
| Yeye a**ta**pika chakula | Yeye hatapika chakula |
| Sisi tu**ta**pika chakula | Sisi hatutapika vyakula |

| | |
|---|---|
| Nyinyi m**ta**pika chakula | Nyinyi hamtapika vyakula |
| Wao wa**ta**pika chakula | Wao hawatapika vyakula |

**TANBIHI:**

1. Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vitakavyofanyika wakati utakaokuja baadaye (future tense)
2. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ ta+ kitenzi kilichopoteza (ku).
3. Maneno yanayoonyesha wakati ujao ni: **kesho, keshokutwa, mtondo, mtondogoo**, n.k

### ❖ WAKATI ULIOPITA (-LI-)

Viambishi wakati katika wakati uliopita ni –**li**- katika hali yakinishi na -**ku**- katika hali ya kukanusha. Wakati huu, hutumika kwa kueleza vitendo vilivyofanyika zamani (past tense). Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ li+ kitenzi kilichopoteza (ku). Maneno yanayoonyesha wakati uliyopita ni: Jana, juzi, juzijuzi, majuzi yale.

Mfano:

Kitenzi: kupika

| Tungo ya kinishi | Tungo kanushi |
|---|---|
| Mimi nilipika chakula | Mimi sikupika chakula |
| Wewe ulipika chakula | Wewe hukupika chakula |
| Yeye alipika chakula | Yeye hakupika chakula |
| Sisi tulipika chakula | Sisi hatukupika vyakula |
| Nyinyi mlipika chakula | Nyinyi hamkupika vyakula |
| Wao walipika chakula | Wao hawakupika vyakula |

### ❖ WAKATI ULIOTIMILIKA (-ME-)

Katika wakati uliotimilika tungo yakinishi, kiambishi wakati ni **-me-.** Katika wakati uliotimilika, tungo kanushi, kiambishi wakati ni **-ja**-. Maneno yanayoonyesha wakati timilifu ni **leo** na **hivi punde.**

**Mfano:** Kitenzi: kufungua

| **Tungo yakinishi** | **Tungo kanushi** |
|---|---|
| Mimi ni**me**fungua chupa | Mimi si**ja**fungua chupa |
| Wewe u**me**fungua chupa | Wewe hu**ja**fungua chupa |
| Yeye a**me**fungua chupa | Yeye ha**ja**fungua chupa |
| Sisi tu**me**fungua chupa | Sisi hatu**ja**fungua chupa |
| Nyinyi m**me**fungua chupa | Nyinyi ham**ja**mefungua chupa |
| Wao wa**me**fungua chupa | Wao hawa**ja**fungua chupa |

**TANBIHI**:

**1**. Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua Kiambishi nafsi huru+ kiambishi nafsi ambatano+ **me**+ kitenzi kilichopoteza (ku).

- **WAKATI WA MAZOEA (HU-)**

Katika wakati wa mazoea, kiambishi **-hu-** huchukua nafasi ya kiambishi nafsi na kiambishi wakati. Wakati wa mazoea humaanisha kutendeka kwa tendo kila siku au kila wakati. Katika kukanusha ni kama vile katika wakati uliopo.

**Mfano:** Kitenzi kutandika

| **Hali yakinishi** | **Hali kanushi** |
|---|---|
| Kila siku mimi hutandika kitanda | Kila siku mimi sitandiki kitanda |
| Kila siku wewe hutandika kitanda | Kila siku wewe hutandiki kitanda |
| Kila siku yeye hutandika kitanda | Kila siku yeye hatandiki kitanda |
| Kila siku sisi hutandika vitanda | Kila siku sisi hatutandiki vitanda |
| Kila siku nyinyi hutandika vitanda | Kila siku nyinyi hamtandiki vitanda |
| Kila siku wao hutandika vitanda | Kila siku wao hawatandiki vitanda |

**TANBIHI** :

Kuweka kitenzi katika hali yakinishi ni kuchukua kiambishi nafsi huru+ **hu**+ kitenzi kilichopoteza (ku). Hali kanushi ni kama wakati uliopo.

[3.2] ***https://swa.gafkosoft.com/nyakati***

## Kazi 2 : Mwongozo wa kivitendo

**Kazi: Andika sentensi hizi katika hali kanushi**

a. Mimi nitarejea Musanze siku ya Ijumaa

b. Tumemkuta hivi punde

c. Wote walimzuru Hospitalini

d. Kamugisha anaandika barua ya kuhudhuria mkutano wiki itakayokuja.

**e.** Wakristo wote husherehekea Sikukuu ya Krismasi kila tarehe 25 Disemba.

**Kazi 3: Utendaji**

**Kazi :** 1. Katika makundi, tungeni sentensi tano za hali kanushi.

## Mada 3.3: Kauli za Vitenzi katika Kiswahili

### Kazi 1 : Utatuzi wa matatizo

**kazi**

1. Katika jozi, wanafunzi wajadili kuhusu kauli za vitenzi ka kuzitumia katika sentensi.

**Mambo Muhimu (Yaliyomo elekezi)**

- **KAULI ZA VITENZI**

Kuna kauli mbalimbali za vitenzi kama ifuatavyo:

✓ **Kauli ya kutenda**

Kauli hii huwakilisha vitenzi katika hali ya hawaida. Hapa kitenzi huwa ni shina la kitenzi bila kuongezwa viambishi vingine vyovyote.

Kwa mfano Lima lim-a

Lala lal-a

✓ **Kauli ya kutendea**

Kauli hii huonyesha kuwa kitendo ni kwa manufaa au kwa niaba ya au kwa faida ya mtu au kitu kingine. **Mofu ya kauli hii ni -i- na -e-.**

Huwa -i- ikiwa mzizi wa kitenzi una vokali /i, a, u/.

Kwa mfano: Pigia pig-i-a

Rukia ruk-i-a

Huwa -e- ikiwa mzizi wa kitenzi una vokali /o, e/.

Kwa mfano: Chomea chom-e-a

Semea sem-e-a

Mofimu hizi pia huwa na alomofu {-liw-, -lew-}. Huwa {-li-} ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia kwa vokali/i, u, a/.

Kwa mfano : Kimbilia kimbi-li-a

Kalia ka-li-a

Chukulia chuku-li-a

Sauti /l/ ambayo imeongezwa hapa ni /l/ ya kuvunja mfuatano wa vokali ili neno likubali muundo wa silabi unapendelewa na lugha za kibantu kama Kiswahili. Inaaminika, kwa mfano kuwa muundo wa ndani na ambao ndio muundo asilia wa neno "zaa" ni [zala] hivyo lingekuwa *zala

Zalia za-li-a hii ingekuwa vivyo hivyo kwa vitenzi tulivyorejelea hapo juu.

- ✓ **Kauli ya kutendwa**

Kauli hii huwakilishwa na mofu {-w-} katika Kiswahili. Hali hii inaamanisha kuwa mtu au kitu kimefanywa kitu.

**Kwa mfano:** pigwa pig-w-a

- ✓ **Kauli ya kutendewa**

Kauli hii humaanisha hali ya kutenda kitendo kwa niaba ya mhusika fulani. Athari za kitendo cha namna hii huwa kwa anayetendewa kitendo. Mofu ya kauli hii ni {-iw-} na huwa na alomofu {-ew-,-liw-,-lew-}. Sababu za kuwepo na alomofu hizi zinatokana na harakati za kifonolojia kama tulivyoeleza katika kauli ya kutendea.

**Kwa mfano**: Limiwa lim-iw-a

Chomewa chom-ew-a

Jadiliwa jadi-liw-a

Tembelewa tembe-lew-a

- ✓ **Kauli ya kutendeka**

Kauli hii huwakilisha uwezekano wa kitendo kufanyika. Mofimu ya kauli hii huwakilishwa no mofu {-ik-} na alomofu zake {-ek-,-lik-,-lek-}. Hii husababishwa na muundo wa mzizi wa kitenzi kama tulivyoeleza hapo awali.

**Kwa mfano:** imbika imb-ik-a

Semeka sem-ek-a

Kimbilika kimbi-lik-a

- ✓ **Kauli ya kutendesha**

Kauli ya kutendesha huwa na maana ya usababishi. Usababishi huu huweza kuwa ama mhusika au wahusika fulani wanasababisha kufanyika kwa kitendo na mhusika au wahusika wengine, au mhusika au wahusika wengine wanafanywa kutenda kitendo na mhusika au wahusika fulani. Mofu ya mofimu hii ya usababishi huwa {-ish-} na huwa na alomofu {-esh-,-lish-,-lesh-,-iz-,-ez-}.

Huwa {-ish-} ikiwa mzizi wa kitenzi waishia kwa konsonanti na una vokali /i, u, a/.

Kwa mfano: limisha lim-ish-a

Lalisha lal-ish-a

Huwa {-esh-} ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia kwa konsonanti na una vokali /o,e/

**Kwa mfano:** Ogesha og-esh-a

Jengesha jeng-esh-a

Huwa {-lish-} ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia kwa vokali ambayo ni kati ya /a, u, i/.

**Kwa mfano:** tambulisha tambu-lish-a

Huwa {-lesh-} ikiwa mzizi wa kitenzi kinachohusika huishia kwa vokali na una vokali /o, e/.

**Kwa mfano:** Tobolesha tobo-lesh-a

Zolesha zo-lesh-a

Wakati mwingine mofimu usababishi huwakilishwa na mofu {-iz-} ikiwa mzizi unaishia kwa vokali na kama una vokali i, u au a. Mofu {-ez-} pia hudhihirika ikiwa mzizi unaishia kwa vokali na mzizi una ama vokali e au o.

Tembeza tembe-ez-a

Kimbiza kimbi-iz-a

- ✓ **Kauli ya kutendana**

Kauli hii hurejelea hali ambapo wahusika hufanyiana kitendo, huyu akamfanya Yule na wakati huo huo yule akamfanya huyu. Athari za kitendo huwa kwa pande zote mbili. Kauli hii huwakilishwa kwa kiambishi {-an-} katika Kiswahili. Kinyume na mofu za kauli za hapo awali mofu hii hudhihirika vivyo hivyo katika mazingira yote ambamo inatokea katika Kiswahili.

Kwa mfano: Pendana pend-an-a

Chomana chom-an-a

Katana kat-an-a

- ✓ **Kauli ya kutendama**

Kauli hii hurejelea hali ambapo watu au kitu hukaa pamoja kwa muda mrefu. Mofu ya kauli hii katika Kiswahili huwa {-am-}

Kwa mfano: fungama fung-am-a

Gandama gand-am-a

- ✓ **Kauli ya kutendata**

Hali nyingine ambayo inakaribiana nay a kutendama ni ile ya kuwa pamoja. Mofu {-at-} ndiyo inayowakilisha mofimu ya kuwa pamoja.

Kwa mfano: fumbata fumb-at-a
Vitenzi vinavyochukua hali hii ni vichache katika Kiswahili.

- ✓ **Kauli ya kutendua**

Hii ni kauli ambayo huonyesha kinyume cha kitendo. Mofimu ya kauli hii huwa na mofu {-u-} na {-o-}. Kwa mfano: zibua zib-u-a

Chomoa chom-o-a

Fungua fung-u-a
Wakati shina la kitenzi linaporudiwarudiwa, tunasema huo ni uradidi. Hali hiyo inaonyesha kuwa kitendo kimefanyika kwa muda mrefu au kwa njia isiyofaa.

Kwa mfano: Anatembeatembea a-na-tembe-a-tembe-a

| | |
|---|---|
| Anarukaruka | a-na-ruk-a-ruk-a |
| Anaimbaimba | a-na-imb-a-imb-a |

- ✓ **Kauli ya kujirejea**

Kauli ya kujirejea huhusu uhusiano wa kitenzi na kiima tu bila kuhusisha yambwa.

**Mifano:**

- Paulo amejikata
- Daudi amejiumiza
- Juma alijipikia chakula

## Kazi 2 : Mwongozo wa kivitendo

**Kazi: Kwa kuongozwa na mwalimu, kamilisha jedwali lifuatalo:**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Pika | Pikwa | pikika | pikikisha | pikia | pikiana |
| Fungua | | | funguza | | |
| Pata | Patwa | | | | |
| Vunja | | | | | vunjana |
| Beba | | bebesha | | | |
| Acha | Achwa | | | | |
| Cheza | | | | | Chezeana |
| Chinja | | chinjika | | | |
| Fahamu | | | | | |
| Linda | | | | | |
| Fuga | | | | | |

## Kazi 3 : Utendaji

**Kazi:** Katika makundi ya wanafunzi watano, bainisha sentensi tano zenye kauli za vitenzi.

## Tathmini Endelezi

**I. Weka vitenzi vilivyo mabanoni katika wakati unaofaa**

a) Muhire ………………… (fanya) mtihani wa taifa kesho asubuhi.

b) Abimana …………….. (rejea) shuleni) leo asubuhi.

c) Kagaba ……. (jenga) nyumba kila wiki.

d) Wanakulima ……………… (Panda) mahindi sasa hivi.

e) Siku zilizopita, Sangwa …………..(faulu) vizuri somo la Hisabati.

**II. Kanusha sentensi zifuatazo**

a) Niyigena alipuuza somo la Kemia.

b) Uwindekwe amerejea nyumbani kwao.

c) Manigabe ataleta sufuria ya kupikia uji.

d) Mutesi anahudhuria kongamano la Kiswahili.

e) Kabalisa hupenda kusali kila Ijumaa.

III. Andika vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendua (kinyume cha vitenzi hivi chini)

a. Kupanga:…..
b. Kutatiza:…….
c. Kunasa:……
d. Kufumba:…
e. Kutega:……
f. kujenga:…
g. Kuezeka:……
h. Kuficha:……..
i. Kubandika:……
j. Kuanika:……
k. Kukunja:…….
l. Kutandika:
m. Kukwama…
n. Kushona……
o. Kuumba:….
p. Kupakia……..

**IV. Weka vitenzi vinavyokolozwa katika kauli iliyotajwa katika mabano**

b. Kalisa anapenda Kamali (kauli ya kutendana)
c. Agaba anafundisha Hisabati (Kauli ya kutendwa)
d. Muhire anasoma Kiswahili (Kauli ya kutendesha)
e. Chai inalpikwa sasa hivi (kauli ya kutendeka)
f. Karangwa anapika chapati (kauli ya kutendatenda)

## Mambo ya kukumbuka (Vidokezo muhimu)

**Vidokezo muhimu vinavyojitokeza katika mada hii ni**

- Kauli ya kutenda,
- Kauli ya kutendana
- Kauli ya kutendeka
- Kauli ya kutendesha,
- Kauli ya kutendewa
- Kauli ya kutendwa,
- Kauli ya kutendeana
- Kauli ya kutendatenda
- Kauli ya kutendana
- Kauli ya kujirudia n.k...

## Kujitafakari

**Tahmini ya baada ya Ujifinzaji na Ufundishaji**

- Jaza tathmini ya kibinafsi hapa chini.
- Hakuna njia sahihi au zisizo sahihi za kujibu utafiti huu.
- Ni kwa matumizi yako mwenyewe wakati wa kozi hii.
- Fikiria juu yako mwenyewe : unafikiri unaweza kufanya hivi ? Vipi vizuri?
- Soma taarifa hizo hapo chini.
- Weka tiki kwenye safu inayowakilisha vyema hali yako

| **Uzoefu wangu**<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuainisha nyakati tofauti katika Kiswahili | | | | | |
| Kutumia nyakati tofauti katika mazungumzo maandishi | | | | | |
| Kujenga mawasiliano mema katika mazungumzo | | | | | |
| Kutofautisha matumizi ya hali yakinishi na hali kanushi katika | | | | | |

| Uzoefu wangu<br><br>**Maarifa, stadi na maadili** | **Sina uzoefu wowote wakufanya hivi** | **Ninajua kidogo kuhusu hili.** | **Nina uzoefu wa kufanya hivi** | **Nina uzoefu kutosha kuhusu hili** | **Ninajiamini katika uwezo wangu wa kufanya hivi.** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mazungumzo na maandishi | | | | | |
| Kutumia vema hali kanushi na hali yakinishi | | | | | |
| Kutaja kauli mablimbali za vitenzi | | | | | |
| Kutumia kauli tofauti katika mazungumzo | | | | | |

## Kujitafakari

Jaza jedwali hapa chini na ushirikishe matokeo na mwalimu kwa mwongozo zaidi.

| **Maeneo** Februari **ya uimarishaji** | **Maeneo ya uboreshaji** | **Vitendo vinavyotakiwa ili kuboresha** |
|---|---|---|
| **1.**<br><br>**2.** | **1.**<br><br>**2.** | **1.**<br><br>**2.** |

## Upimaji wa Jumla

1. **Toa majibu ya maamkizi yafuatayo**
    a) Chewa?
    b) Shikamoo?
    c) Je, wanao hawajambo?
    d) Usiku mwema!
    e) Habari ya jioni?
2. **Andika nambari hizi kwa maneno**
    a) 4/5
    b) 567
    c) 467.543
    d) 76%
    e) 467.543
3. Orodhesha siku za wiki
4. Taja aina tatu za mavazi
5. Taja aina tatu za usafiri
6. **Kamilisha sentensi zifuatazo hizi kwa kutumia neno moja kati ya yaliyopendekezwa ndani ya mabano**.
    a) Ukurasa.......... (moja, mmoja, wamoja, kumoja) ............ (kinatosha, wanatosha, unatosha)
    b) Chumba........................................................ (yetu, wetu, chetu, zetu) ........... (Kinafunguliwa, wanafunguliwa, inafunguliwa, zinafunguliwa).
    c) Kikapu ..................... (hiki, hii, hawa, yule) .............................. (amejaa, kimejaa, vimejaa) vitu.
    d) Nyimbo..................... (zitatu, tatu, ntatu) ................................ (zinaandikwa, vinaandikwa, wnaandikwa).
    e) Visu...... (zenu, vyenu, chenu, zetu) .......................... (vinatoa, kinatoa, zinotoa, inatoa).

7. **Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viunganishi vinavyofaa kati ya vile vilivyopendekezwa katika mabano.**
   a) Mwalimu anatuomba tufute ubao…………aandike zoezi la Kiswahili (ili, pamoja, au).
   b) Mwanafunzi huyu anafaulu mtihani……………………………….anajifunza vizuri (kwa sababu, ili, au).
   c) Yeye anajenga nyumba hii …………. (Ili, kwa, kwa sababu) mawe ………… (isipokuwa, na, vilevile) matofali.
   d) Wananchi wanaheshimiana …. ………wanasaidiana katika shughuli zao za kila siku (na, ili, kwa sababu).
8. **Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kitenzi kinachofaa katika wakati uliopita tungo kanushi.**
   a) Watoto hawa ………. (kuchora) picha nzuri.
   b) Mimi………………. (teka) maji ya kupika.
   c) Yeye……………(kununua) mkate siku ile.
   d) Ng'ombe wake …………. (kutibiwa) ugonjwa ule.
   e) Mbuzi wote…………………. (kuuzwa)sokoni.
9. **Zijaze nafasi tupu katika jeduali:**

| 1.piga | pigwa | pigika | pigisha | pigia | pigana |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.pika | …… | pikika | …….. | ……… | …….. |
| 3.andika | andikwa | ……. | ……. | ……. | ……. |
| 4.Lima | ……. | …….. | limisha | …….. | …….. |
| 5.Fua | ……. | ……. | …….. | …….. | ……. |
| 6.penda | pendwa | ……. | ……. | ……. | ……. |
| 7.pita | …….. | …… | ……. | …… | Pitana |
| 8.Funga | …… | …… | fungisha | …… | ……. |
| 9.Sikia | ……. | sikika | …….. | ……. | …….. |
| 10.Rarua | ……. | ……. | ……. | rarulia | ……. |

# MAREJELEO:


1. Ahmed, N. (1997). Mwangaza wa Kiswahili, Nairobi, East African Educational Publishers.
2. BAKITA (2014). Kamusi ya Karne ya 21, Dar es Salaam, Longhorn Publishers.
3. Goamolloh N. (2007). KCPE Revision Kiswahili, Nairobi, The Creative Print House Limited
4. Hassan O. Ali& Ali Mazrui (2004). Teach yourself Swahili. Nairobi: Oxford University Press.
5. Kihore, Y.M, Massamba, D.P.B, Msanjila, Y. P. (1999). Sarufi Maumbo ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo.Dar es Salaam.
6. Masamba, Kihore&Hokororo (2001). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Dar- Es-Salaam.TUKI
7. Nkwera F.V.M. (1985). Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo. Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.
8. Ntawiyanga, S. &Kinya, J.M, (2016). Kiswahili kwa Shule za Rwanda: Kitabu cha Mwanafunzi, kidato cha Pili, Kigali, Longhorn Publishers
9. TUKI (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar Es Salaam: Oxford University Press
10. Wamitila, K.W. (2003). Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focas Book

RTB | RWANDA TVET BOARD

Februari, 2023